# Tujibu Mashahidi Wa Yehova Mstari Kwa Mstari.

**Kimetolewa na**
**Ndugu Heath Stapleton**

# Yaliyomo


| Sura | Sehemu Ya Sura | Ukurasa |
|---|---|---|
| Sura Ya Kwanza | Historia Kwa Ufupi | 4-5 |
| Sura Ya Pili | Historia Ya Muda | 6 |
| Sura Ya Tatu | Mafundisho Ya Mashahidi | 7-18 |
| | I. Kulisifu Jina La Mungu | 7-8 |
| | II. Kanisa Na Ufalme | 8 |
| | III. Jehanum Na Roho Kuangamizwa | 8-9 |
| | IV. Vitabu Vyao | 9-10 |
| | V. Nafsi Moja Tu | 10-12 |
| | VI. Kuhusu Yesu | 12-14 |
| | VII. Nafasi Ya Pili Kuokolewa | 14 |
| | VIII. Chakula Cha Bwana | 14-15 |
| | IX. Ukombozi Uliaanza 1874 bk. | 15 |
| | X. Mavuno Ya Injili Yamekwisha | 15 |
| | XI. Roho Mtakatifu Si Nafsi | 16 |
| | XII. Hatufi Kwa Dhambi Zetu | 16 |
| | XIII. Utawala Wa Miaka 1000 | 17 |
| | XIV. Msalaba | 17 |
| | XV. Tunaokolewa Kwa Imani Tu! | 18 |
| Sura Ya Nne | Agano La Kale | 19-28 |
| | Mwanzo 1:1-2 | 19 |
| | Mwa. 9:4 | 19-20 |
| | Mwa. 18:1-2 | 20-21 |
| | Mwa. 40:20-22 | 21 |
| | Kutoka 3:14 | 21 |
| | Kut. 3:15 | 21 |
| | Kumbukumbu La Torati 18:20-22 | 21-22 |
| | Zaburi 37:9, 11, 29 | 22-23 |
| | Zab. 110:1 | 23-24 |
| | Zab. 146:3-4 | 24 |
| | Mhubiri 9:5, 10 | 24-25 |
| | Isaya 9:6 | 25-26 |
| | Isa. 43:10 | 26 |
| | Ezekieli 18:4 | 26-27 |
| | Danieli 10:13, 21; 12:1 | 27-28 |
| Sura Ya Tano | Agano Jipya | 29-50 |
| | Mathayo 3:11 | 29 |
| | Mat. 6:9 | 29-30 |
| | Mat. 14:6-10 | 30 |

| | | |
|---|---|---|
| | Mat. 24:3 | 30-31 |
| | Mat. 24:14 | 31-32 |
| | Mat. 24:34 | 32 |
| | Mat. 24:45-47 | 32-33 |
| | Mat. 26:27 | 33-34 |
| | Marko 1:8 | 34 |
| | Marko 6:21-25 | 34 |
| | Marko 12:29 | 34 |
| | Luka 3:16 | 34 |
| | Lk. 16:22-24, 27-28 | 34-35 |
| | Lk. 22:19 | 35 |
| | Lk. 22:43 | 35-36 |
| | Lk. 24:36-39 | 36 |
| | Yohana 1:1 | 36-37 |
| | Yoh. 3:3, 7 | 37 |
| | Yoh. 4:23 | 38 |
| | Yoh. 6:53 | 38 |
| | Yoh. 8:58 | 38 |
| | Yoh. 10:16 | 38-39 |
| | Yoh. 14:28 | 39-40 |
| | Yoh. 16:13 | 40 |
| | Yoh. 17:3 | 40-41 |
| | Yoh. 20:25 | 41 |
| | Yoh. 20:28 | 41-42 |
| | Matendo 1:5 | 42 |
| | Mdo. 2:4 | 42 |
| | Mdo. 5:3-4 | 42-43 |
| | Mdo. 7:59-60 | 43 |
| | Mdo. 15:28-29 | 43 |
| | Warumi 8:8-9 | 43 |
| | Warumi 8:26-27 | 43 |
| | 1 Wakorinto 1:10 | 43-44 |
| | 1 Kor. 6:19 | 44 |
| | 1 Kor. 8:6 | 44-45 |
| | 1 Kor. 11:7 | 45 |
| | Wakolosai 1:15 | 45 |
| | Kol. 2:9 | 45-46 |
| | 2 Timotheo 3:15-17 | 46 |
| | 2 Petro 1:3 | 46 |
| | Waebrania 1:6 | 46 |
| | Ufunuo 1:7-8 | 46-48 |
| | Ufu. 3:14 | 48 |
| | Ufu. 7:4 | 48-49 |
| | Ufu. 7:9; 19:1 | 49 |
| Sura Ya Sita | Hitimisho | 50 |

# Sura Ya Kwanza

## Historia Kwa Ufupi

1. Charles Taze Russell (1854-1916) wa Marekani alianza kufundisha watu kwamba Yesu yu karibu kusimamisha ufalme wake. Katika mwaka 1872 bk. wafuasi wake waliunda chama cha ushirika.

2. Kabla ya kuhubiri ya kuwa Yesu atarudi katika mwaka wa 1874 bk., Ndugu Russell alikuwa Msabato. Lakini alipinga mafundisho ya William Miller kuhusu Yesu atarudi lini, na alianza kufundisha mafundisho yake ya kuwa Yesu atarudi lini.

3. Aliweka mkao mkuu Pittsburgh, Pennsylvania mwaka wa 1872, na alifanya yeye mwenyewe awe rahisi. Katika mwaka wa 1909 alihamisha mkao mkuu mpaka Brooklyn, New York.

4. Lakini hawakuitwa Mashahidi wa Mungu mpaka mwaka 1931. Wanadai mashahidi walikuwepo duniani tangu siku za Habili na wanadondoa Isa. 43:10-12; Ebr. 11; na Yn. 18:37 kama ni uthibitisho wa imani yao.

5. Charles Taze Russell aliandika vitabu sita vinaitwa, <u>Studies In The Scriptures.</u> Vitabu vile vilijenga msingi wa imani ya Mashahidi.

6. Rusell alikufa mwaka wa 1916 na Joseph Rutherford alichaguliwa awe rais wao wa chama cha uchapaji kinachoitwa Watchtower Bible and Tract Society.

7. Rutherford aliandika vitabu vingi vinavyoeleza imani yao. Na ndio yeye aliyeandika kwamba, "**watu mamilioni wanaoishi sasa hawatakufa**." Alikuwa na mana kwamba Yesu atarudi **karibuni**. Walakini Rutherford mwenyewe alikufa mwaka 1942 na mpaka sasa Yesu hajarudi!

8. Yeye alifundisha kwamba Yesu aliaanza kutawala mwaka 1914 na alitakasa hekalu la Mungu mwaka wa 1917. Na alitufundisha ya kuwa tutakuwa na vita kuu (Har-Magedoni) na ndipo Yesu atakuja kwa watu wake.

9. Bada ya kifo cha Rutherford ndugu N. H. Knorr alichaguliwa awe rais, 1942.

10. Katika mwaka wa 1950 waliandika tafsiri yao wenyewe ya Biblia inayoitwa "New World Translation", wakasema ni tafsiri iliyo sahihi.

11. Pia mwanzilishi wao (Russell) alikuwa **MHUNI** sana, sio kidogo lakini **SANA**! (Aliyeanzisha madhehebu ya Mashahidi na kuandika vitabu sita vinavyoitwa "Majifunzo Ndani ya Maandiko".) Katika kitabu cha "Churches of Today" uk. 97, tunaambiwa yafuatayo: "Alipelekwa mahakamani na mkewe akishitakiwa kuwa ni mzinzi! Kortini, alikiri mwenyewe kwamba **alikuwa na wapenzi wengi.** Basi, serikali iliamua kuwa ni haki kwa mkewe apewe talaka na kumwacha. Tena, serikali ilimwamuru Russell ampe mkewe fidia. Russell alidai kuwa hana fedha. Lakini, serikali ilipeleleza mambo yake ikagundua kuwa alikuwa na fedha za Marekani $317,000 ambazo alikuwa amezificha kwa ujanja! Hivyo, alishitakiwa na serikali kuwa ni mwongo!"

Kwa hiyo mwanzilishi wa Mashahidi ni Mwasherati, Mwongo na Mwizi!  Sasa leo watu wana mwaminije huyo mwongo?

# Sura Ya Pili

## Historia ya Muda

1879 Charles Taze Russell alianza kuchapa gazetti Zion's Watch Tower na Herald of Christ's Presence.

1881 Walianzisha Watchtower Tract Society.

1886 Russell alichapa kitabu chake Divine Plan of the Ages (Mpango wa Mungu Kwa Vizazi).

1914 Vita vya Mageddon haikutimia kama walivyotabiri.

1916 Charles Russell alifariki.

1917 J. F. Rutherford alichukua nafasi ya Russell.

1920 Watch Tower walidai watu mamillioni wanaoishi sasa hawatakufa! Tena walitabiri ufufuo wa ulimwengu huu katika mwaka wa 1925.

1925 Watu kama Ibrahimu, Isaka na Yakobu hawakufufuka kama walivyotabiri.

1930 Walijenga nyumba "Beth Sarim" kule San Diego, California U.S.A. kwa ajili ya manabii wa zamani wa Mungu. Walidai manabii wa zamani watafufuka na watahitaji sehemu ya kuishi.

1931 Walichagua jina "Mashahidi wa Yehova" kwa mara ya kwanza.

1942 Rutherford alikufa. N. H. Knorr alichukua nafasi yake.

1950 Walianza kuchapa tafsiri yao ya maandiko, New World Translation. Walimwita Yesu kuwa mungu kati ya miungu mingi. Tena waliongeza neno "Yehova" kwenye Agano Jipya.

1968 Kwenye Watch Tower waliandika kwamba inawezekana Yesu atarudi katika mwaka wa 1975.

1975 Yesu hakufika.

# Sura Ya Tatu

## Mafundisho ya Mashahidi

**Mafundisho ya Mashahidi:**

***I.*** *Kulisifu Jina la Mungu.*

Wanasisitiza sana jina "Yehova" kuwa jina la Mungu (Kut. 6:3-6). Wanasema ni lazima tulisifu jina la Jehovah wakidondoa Zab. 68:4.

**Biblia Yasema Nini?**

1. Agano la Kale liliandikwa katika lugha ya Kiebrania. Alfabeti ya Kiebrania ya asili haikuwa na vokali bali konsonati tu. Walakini, haiwezikani kutamka neno bila kutamka vokali. Kwa hiyo, ilikuwa lazima msomaji wa Kiebrania atambue jinsi ya kutamka maneno kusudi aweze kusoma Kiebrani. Basi, jina la Mungu liliandikwa "YHWH" katika Kiebrania. Mashahidi wanaamini kuwa inatakiwa Wakristo watumie jina hili la Mungu siku zote. Lakini, Waisraeli waliamini kwamba jina hili la Mungu lilikuwa takatifu na kwamba wanadamu wasingelitamka. Kwa sababu ya Kum. 5:11. Kwa hiyo walikataa kusema jina la Mungu hata kama walikuwa na somo maandiko! Kwa hiyo walizoea kutumia jina "Adonai" badala la "YHWH". Lakini kuna mahali kwenye Agano la Kale maneno yote mawili yako pamoja. Ilipotokea hivyo walitamka jina lingine, "Elohim".

Baada ya karne nyingi kupita. Waisraeli hawakuweza kujua vokali za jina la Mungu. Kwa hiyo walichukua herufi "a" toka kwa "Adonai" na helufi "e" toka kwa "Alohim" wakafanya jina "***YAHWEH***". Sasa katika Biblia ya Kilatini jina hili iliandikwa "Yehova". Na jina lililoingizwa katika Biblia ya Kiingereza na ya lugha nyingine nyingi. **Sasa Mashahidi wanasema ni lazima tutumia jina "Yehova"! Kumbe! hatuna hakika kwamba ndio matamko ya halali. Ni jina lililotengenezwa na WANADAMU!** Sasa kama ni muhimu kwetu tujue na kutamka jina la Mungu kwa nini Mungu hakukhakikisha kwamba tunaongea au tunatamka ya kweli.

2. Pia kuna majina mengine ya Mungu katika Kut. 3:14 na Zab. 68:4. Kwa nini Mashahidi hawasisitizi tuyatumie majina hayo? Kwa nini wanataka kutumia "YHWH" tu?

3. Wakristo hawakupewa jina "Mashahidi" wala "YHWH" kwa wokovu wao. Kaitka Isa. 62:2, Mungu alisema atakupa jina jipya. Sasa jina jipya ni "MKRISTO" au "Mashahidi wa Yehova". Angalia Mdo. 11:26; 4:12. Tena huwezi kusoma habari ya Mkristo ye yote aliyetaja hilo jina "Yahweh".

4. "Mashahidi" ni "wale **walioona** jambo." Mitume walikuwa mashahidi, Mdo. 1:3, 8. Hakuna mtu leo aliyemwona haya, Mdo. 1:21-22. Tena hakuna "Mashahidi wa Mungu", kwani **hakuna mwanadamu aliyewahi kumwona Mungu!** Tunaamini Mungu yupo kupitia imani.

5. Bila shaka Yesu alijua jinsi ilivyotakiwa kumsifu Mungu. Sasa Yesu alimwita Mungu "Yehovah"! **Hata siku moja**!

6. Kama Wakristo tulimwambia jinsi ya kumsifu Mungu (Flp. 1:10-11; Efe. 1:6, 12, 14; 1 Pet. 4:11. Mistari hii yote inaonyesha kwamba Wakristo wamsifu na kumtukuza Mungu kwa njia ya Maisha yao, wala si kwa maneno tu ya kumwita YEHOVA! Neno YEHOVA umetengenezwa na HEKIMA YA WANADAMU-1 Kor. 2:5; Yer. 17:5-7!

**Mafundisho ya Mashahidi:**

***II.*** *Kanisa na Ufalme.*
Wanafundisha kwamba ufalme wa Yesu haukuwapo siku za mitume.

Wengine walisema kwamba Yesu alikuja kuusimamisha ufalme wake ila alishindwa kwa sababu watu hawakumpokea kuwa mfalme. Kwa hiyo, akaamua kujenga kanisa badala ya ufalme.

Walitabiri kwamba Yesu atarudi duniani mwaka 1914 kusudi ausimamishe ufalme. Walakini, Yesu hakuonekana mwaka 1914. Basi, ndipo walipoanza kusema eti amerudi kisiri watu wasimwone kwa macho!!!! Nao wanasema ameleta ufalme usioonekana! Wanaamini kwamba Yesu atatawala duniani miaka elfu.

**Biblia Yasema Nini?**

1. Kanisa na ufalme ni mamoja!
Ufu. 1:4-6; Kol. 1:13-14; Ufalme huu ulikuwepo katika KARNE YA KWANZA.

2. Leo watu wanakimbilia katika Yn. 18:36 na Mt. 6:9-13 kufudisha kwamba ufalme bado hujaja! Lakini maana ya Yn. 18:36 iko kwenye Lk. 17:20-21, UFALME WAKE NI WA KIROHO. Na katika Mt. 6 Yesu *aliomba kabla hajaujenga ufalme wake***.** Soma 1 The. 2:12.

3. Tena ufalme unaitwa wa Krsito kwa sababu ufalme huo unatawaliwa na Kristo, Kol. 1:13; Efe. 5:5. Petro alisema “Mungu amemfanya Yesu huyo mliyemsulubisha **kuwa Bwana na Kristo**” Mdo. 2:36. Maana yake ni kwamba hivi
sasa Kristo ni mfalme, Dan. 7:13; Ufu. 5:8-10.

**Mafundisho ya Mashahidi:**

***III.*** *Jehanum na Roho Kuangamizwa*

Mashahidi wandai kwamba hakuna Jehanum. Wanasema mwovu anpokufa, basi anapotea moja kwa moja tu! Wanadondoa Mhu. 3:20-21; 12:7.

**Biblia Yasema Nini?**

1. Ni kweli mwili wa mtu hurudi mavumbini anapokufa, Mwa. 3:19. Lakini mwanadamu si mtu tu! Mwanadamu ni nafsi ya roho pia, maana tumeumbwa kwa mfano wa Mungu, (Mwa. 1:26) naye Mungu hana mwili bali ni roho (Yn. 4:24; Lk. 24:39). Miili ya wandamu wote itarudi mavumbini hata wakiwa wema au waovu. Lakini roho za mwanadamu ndizo zitakazoishi milele ama pamoja na Mungu ama katika Jehanum.

2. **Kifo Cha Roho-**Kifo maana yake ni utengao. Ukitenga roho na mwili basi mwili umekufa, Yak. 2:26. Vivyo hivyo, ukitenga roho na Mungu aliye uhai wetu, basi roho nayo imekufa. (Mungu hakumwambia Adamu uongo aliposema "Siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika" Mwa. 2:17. Adamu hakufa kimwili siku ile bali **alikufa kiroho maana alitengwa na Mungu**, na kufukuzwa katika bustani. Kifo cha roho hakina maana kwamba roho haitakuwapo tena. Roho ni ya milele. Roho ya mwovu inapotengwa na Mungu, basi tunaweza kusema imekufa hata ingawa ili roho bado ipo, 1 Tim. 5:6; Efe. 2:5; Rum. 8:10. Walakini, mtu akifa katika dhambi zake, basi roho ya mwovu yule itakuwa katika hali ya mateso daima mbali na Mungu, 2 The.1:7-9; Mt. 25:41-46. Hii **ndiyo inayoitwa MAUTI YA PILI** na ndiyo kifo cha kiroho, Ufu. 21:8; 20:14-15.

3. Ikiwa hakuna mahali pa mateso panapoitwa Jehanum, **mbona Yesu hakujua**? ***Maana Yesu ametuonya mara nyingi kuhusu Jehanum***, Mt. 10:28; Lk. 12:5; Mt. 5: 22, 29-30; 23:33.

4. Mhu. 3:20-21; 12:7 haisema kwamba hakuna Jehanum. Mistari hii inaonyesha kwamba mwili unarudi mavumbini mtu anapokufa. Lakini, miili yetu haitakaa mavumbini daima. La! bali Yesu atakapokuja, wafu wote watafufuliwa, Yn. 5:28-29; Ufu. 20:12-15. Si vigumu kwa Mungu kufufua miili yetu kutoka mavumbini, Eze. 37:1-13. Isitoshe, mara tutakapofufuliwa miili yetu itabadilishwa kama apendavyo Mungu maana nyama na damu haviwezi kuurithi ufalme wa Mungu, 1 Kor. 15:50-54.

5. Masahidi wanasema kwamba hakuna adhabu ya milele, Soma Dan. 12:2; Mt. 25:46; Yn. 5:28-29; Ufu. 20:10.

**Mafundisho ya Mashahidi**

***IV.*** *Vitabu Vyao*

Mashahidi wanaheshimu vitabu vyao kuliko Biblia. Katika gazeti lao "Watchtower" toleo la 15/9/1910 ukarasa 298 walisifu maandishi yao yanayoitwa "Scripture Studies". Na kusema kwamba hakuna uwezo kwa watu kuelewa mpango wa Mungu kwa kusoma BIBLIA TU, bila kusoma "Scripture Studies". Wakisema hata ikiwa mtu amesoma "Scripture Studies" kwa miaka kumi na kuelewa mengi, akianza kusoma Biblia tu, basi baada ya miaka miwili atakuwa amerudi gizani tena! Siyo haya tu! Hawataki watu wasome tafsiri ya Biblia yo yote isipokuwa yao itwayo "New World Translation".

**Biblia Yasema Nini?**

1. Yn. 16:13-Yesu aliwaahid mitume wataongozwa na Roho Mtakatifu katika ukweli yote! Kwa hiyo kama wameongoza katika ukweli yote tunahitaji zaidi? Hapana!!

2. Pia unabii ulikoma wakati vitabu vyote vya Biblia vilipokwisha kuandikwa.

a) Unabii ulikuwa kwa muda. Katika karne ya kwanza Wakristo hawakuwa na maandiko ya Agano Jipya. Kwa hiyo Mungu aliweka manabii katika mji mbalimbali akawaongoza kwa Roho Mtakatifu ili wakumbuke maneno yote ya Yesu na kuwafundisha watu wa miji ile (1 Kor. 14:26-33). Pia walikuwa na uwezo wa kufanya miujiza na ishara kusudi watu wajue kwamba maneno yao yalitoka kwa Mungu, Yn. 14:26; Mk. 16:20; Mdo. 1:5-8.

b) Mungu alisema unabii utakoma pamoja na ishara zake wakati ijapo ili iliyo kamili, 1 Kor. 13:8-10. "Iliyo Kamili" ni sheria ya Yesu (Agano Jipya) ambayo sasa imeandikwa kwa ukamilifu kusudi watu wote wasome wenyewe (Yak. 1:25; 2 Tim. 3:14-17; Yn. 20:30-31).

c) Hatuhitaji manabii leo wala ishara. Kwanza manabii walijua kwa sehemu tu, 1 Kor. 13:9 bali sasa tunayo maneno yote ya Yesu yanatufaa kabisa! 2 Tim. 3:16-17; Gal. 1:8-9; Efe. 2:20; Yud. 1:3; Mt. 12:38-40; Lk. 16:19-31.

3. "Mwishidanie imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu", Yud. 1:3. Imani imeshafika mara moja tu, kwenye maandiko! Sasa kwa nini tunahitaji zaidi. Na ni wapi Mungu alisema "Utafute manabii na maandiko na maneno zaidi ambayo hayakuwemo kwenye maandiko?"

4. Timotheo aliyajua maandiko matakatifu yaletao **WOKOVU** kwenye karne ya kwanza? 2 Tim. 3:15. Sasa kwa nini tunahitaji zaidi?

5. Watu leo wanazungumza kwamba watu wazima hawawezi kuelewa maandiko lakini Yesu alisema nini katika Mt. 11:25?

6. Tena neno la Mungu latosha sana kuongoza watu! Soma Mt. 22:29. Sasa tuseme kwamba Yesu hajui?

7. Isitoshe tumeaambia tusiongeza lo lote katika yale yaliyoandikwa, Gal. 1:6-9.

8. Wataalamu wa kutafsiri Biblia wanatueleza kwamba tafsiri ya Mashahidi ya Biblia si sahihi kuliko tafsiri nyingine. Wametafsiri wakichagua maneno yanayowasaidia kufundisha imani yao. Angali Mungu asemavyo kuhusu neno lake, "Mkijua neno hili kwanza, ya kwamba hakuna unabii katika maandiko upatao kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani tu. Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu," 2 Pet. 1:20-21. Eti! Mungu hakuwa na uwezo wa kuilinda Biblia ikiwa na makosa kabla ya kuwapo kwa hawa Mashahidi? Je, Mungu alikuwa na upendeleo wa kuwachagua Mashahidi tu awafunulie ukweli? Mungu angekuwa na sababu gani kutuachia tafsiri mbovu ya Biblia miaka yote ya nyuma? Isitoshe, ikiwa kweli ni tafsiri mbovu, mbona Mashahidi wenyewe waliitumia kabla ya mwaka 1950 wakifundisha imani yao?! Ukweli ni kwamba Mungu amekilinda kitabu chake tangu mwanzoni (Isa. 40:8; Mt. 24:35; 1 Pet. 1:23-25). Tumeonywa, "Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli," 2 Tim. 2:15. Si watu wote wanotumia neno la Mungu kwa halali! Pia soma 2 Pet. 3:16.

**Mafundisho ya Mashahidi:**

***V.*** *Mashahidi wanafundisha kuwa kuna nafsi moja tu katika Uungu naye ni Baba tu.*

**Mafundisho ya Biblia:**

**1. Je! Yesu ni yule Mungu mmoja?**

Musa alisema: "Sikiliza, Ee Israeli: Bwana Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja," Kum. 6:4.

Yesu alisema:  “Mimi na Baba tu umoja,” Yoh. 10:30.

Mtume Paula alisema, “Maana katika yeye (Yesu) unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili,” Kol. 2:9.

Sasa Mashahidi wanafundisha kuwa kuna nafsi moja na ni Yehova.  Lakini hapa tumeona nini?  Tumeona kwamba wako wawili sasa.  Lakini kuna wawili tu?  La!  Mafundisho ya Biblia yaliyo wazi sana.

Soma 1 Yoh. 5:8, “Kwa maana **wako watatu** washuhudiao mbinguni, **Baba, na neno, na Roho Mtakatifu,** na watatu hawa ni umoja.”

Tazama, neno la Mungu lasema kuwa **wako watatu mbinguni,** na nafsi hizi tatu hufanya Uungu ule mmoja.  Na maana ya kusema hayo ni sawasaw na maana yake aliposema kuwa duniani kuna “Roho, na maji, na damu;  na watatu hawa hupatana kwa habari moja.” mst. 9.  Na tunaelewa kwamba roho, maji na damu sio kitu kimoja kiasili.  La, bali umoja wao ni ushuhuda wanaotoa kuhusu Yesu.  Vivyo hivyo, Baba, Neno, na Roho Mtakatifu ni nafsi tofauti tatu wanaomshuhudia Yesu kuwa Mwana wa Mungu.  Kuna Mungu moja tu, walakini ana nafsi zake tatu.  Yesu aliposema, “Mimi na Babatu umoja,” hakuwa na maana kuwa Yeye mwenyewe ndiye Baba.

Tena tuangalia 2 Kor. 13:14, maneno hayo ya Biblia yaonyesha kuwa Uungu ni wa nafsi tatu.  Sasa tuchunguza kwenye Biblia maana ya “Umoja” walio nao Baba na Mwana.

Efe.5:29-32, “Maana hakuna mtu anayeuchukia mwili wake po pote;  bali huulisha na kuutunza, kama Kristo naye anavyolitndea Kanisa.  Kwa kuwa tu viungo vya mwili wake.  Kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na mama yake, ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili moja.  Siri hiyo ni kubwa;  ila mimi na nena habari ya Kristo na Kanisa.  Lakini kila mtu ampende mke wake kama nafsi yake mwenyewe;  wala mke asikose kumstahi mumewe.”

Mst. 30 - “Tu viungo vya mwili wake”.
Mst. 31 - “Hao wawili watakuwa mwili moja**.”**

Tazama: 1) Kanisa ni mwili ule mmoja wa Kristo.  Sasa maana ya maneno hayo ya Efe. 5 ni kwamba kanisa ni mtu mmoja tu.  Je, Petro, Paulo, Apollo, Barnaba, Timotheo, Tito na Yohana wote walikuwa mtu mmoja tu?  La, mtume mwenyewe alisema kuwa ni Viungo vya mwili ule mmoja.  Kanisa ni watu mbalimbali tofauti wanaounganishwa washiriki umoja wa kiroho.  Wanashirikiana katika baraka na kazi za Yesu.  Vivyo hivyo, Yesu na Baba wa umoja, hata ingawa ni wawili.

2) Pia mistari hii inasema mume na mkeo ni mwili mmoja tu!  Je, kweli hawa wawili ni mwili mmoja?  Hapana.  Lakini wale wawili ni umoja katika kazi na baraka za ndoa?  Vivyo hivyo Yesu, Baba na Roho ni mmoja; hata ingawa ni watatu.

Yn. 17:20-21 “Wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako:  hao nao wawe ndani yetu.”

Je, umoja ambao Yesu alituombea ni kwamba Wakristo wote wawe mtu mmoja tu?  Si anaongea habari ya umoja wa matendo, imani, na maneno yetu?  Kama vile Yesu na Baba wanao umoja katika kutuumba na

kutuletea wokovu, vivyo hivyo Wakristo wawe na lengo moja na juhudi moja.  Tuone mfano mwengine wa umoja katika Biblia.  2 Sam. 7:23, "Tena ni taifa lipi duniani lililo kama watu wako, kama Israeli...?" Waisraeli walikuwa watu wengi na makabila mengi lakini wanaitwa kuwa ni taifa moja tu!  Vivyo hivyo, Uungu ni mmoja, lakini una nafsi tatu.

**2. Matatizo ya kusema kuna nafsi moja tu.**

Yn. 17:1-5, Maneno hayo aliyasema Yesu; akainua macho yake kuelekea mbinguni, akasema, Baba, saa imekwisha kufika.  Mtukuze Mwanao, ili Mwana wako naye akutukuze wewe;  kama vile ulivyompa mamlaka juu ya wote wenye mwili, ili kwamba wote uliompa awape uzima wa milele.  Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma.  Mimi nimekutukuza dunia, hali nimeimaliza kazi ile uliyonipa nifanye.  Na sasa, Baba, unitukuze mimi pamoja nawe, kwa utukufu ule niliokuwa nao pamoja nawe kabla ya ulimwengu kuwako."

Sasa kama Mungu ni nafsi moja tu, na Mungu alikuja ulimwenguni katika mwili na aliitwa Yesu.  Sasa huyo Yesu (Kama nafsi peke) alikuwa ana ongea na nani hapa?  Mbona alisema, Wakujue wewe, Mungu wa pekee, na Yesu Kristo uliyemtuma.  Akiwa yeye (Yesu) alikuwa nafsi pekee sasa nani alitumwa huyu? Kwa hiyo tumeona Baba na Mwana ni nafsi mbili tofauti.  Na wana umoja katika kazi zao na asili yao ya Uungu.

Soma Yn. 14:9-10, "Yesu akamwambia, Mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote, wewe usinijue, Filipo?  Aliyeniona mimi amemwona Baba;  basi wewe wasemaje, Utuonyeshe Baba?  Husadiki ya kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani yangu?  Hayo maneno niwaambiayo mimi siyasemi kwa shauri langu;  lakini Baba akaaye ndani yangu huzifanya kazi zake."

Sasa wakati Yesu alisema "Siyasemi kwa shauri langu".  Sasa ameyasema kwa shauri la nani?  Akiwa ni nafsi pekee, ni nani aliyempa maneno ayaseme?  Yesu tena alisema, "**Mimi ni ndani ya Baba na Baba yu ndani yangu**."  Sasa hakusema Yeye ni Baba!  Lakini alisema Baba yu ndani yake!  Kwa hiyo 1 + 1=2! Kumbe!

Yn. 14:26, "Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia."

Tazama 1+1+1=3.  Wako Watatu!  Roho Mtakatifu atakayepelekwa na Baba kwa jina la Yesu!  Pia angalia mistari hii:

1 Kor. 11:3; 1 Kor. 15:24-28; 1 Tim. 2:5; Mk. 13:32; Mt. 27:46; Lk. 23:46-47.

**Mafundisho ya Mashahidi:**

***VI.*** *Mafundisho Kuhusu Yesu*

1. Yesu alikuwa Malaika aliyeumbwa.

2. Yesu hakuwa Mungu na mwanadamu wakati ule.

Mashahidi wanasema kuwa Yesu hakuchanganya au kushiriki tabia za kiungu na za kimwili alipokuwa duniani.  Wanadai alipokuwa duniani alikuwa mwanadamu mkamilifu tu.  Na tangu kufufuliwa, yeye ni nafsi kamili ya kiroho tu.

3. Yesu alishindwa kuwakomboa wanadamu.

4. Mwili wa Yesu haukufufuliwa.

5. Mwanadamu Yesu amekufa kwa hiyo haishi tena.

6. Kabla ya kufa Yesu alikuwa mwanadamu tu, bali baada ya kufufuliwa alikuwa na hali ya kiungu (malaika).

7. Yesu si mpatanishi wetu.

**Lakini Biblia Linafundisha Nini?**

1. Yesu si malaika.  Soma-Ebr. 1:1-8.  Yeye ni bora.  Pia soma Yn. 1:1-3; 8:58; Ufu. 1:8; 21:6; 22:13 - Yesu hakuumbwa bali yeye mwenyewe ni mwumbaji aliye wa milele.

2. Isaya alitabiri kwamba Mungu angeishi kimwili-Isa. 7:14;  Mt. 1:23.  Mariamu pia alikuwa na mimba kupitia uwezo wa Roho Mtakatifu, mwili wa Yesu alitoka kwa Mariamu lakini Roho kwa Mungu.  Kwa hiyo Yesu alikuwa asili zote mbili--kimwili na kiroho, Mt. 1:18-20.  Katika Fil. 2:6-7 tunaona kwamba Yesu alifanyiwa kuwa mfano wa Mwanadamu, Flp. 2:6-7;  Ebr. 2:16.  Pia tunaweza kusoma katika Yn. 1:1-2, 14; 16:28;  1 Tim. 3:16.  Pia tunaweza kumwona Petro alikiri katika Mat. 16:18, Yesu ni nani?  Na kama kuna mtu ambaye anatufundisha ya kuwa Yesu hatokani na Mungu, mwambie asome 1 Yoh. 4:3 na 2 Yoh. 7.

3.  Mashahidi wanasema Yesu si mkombozi wetu.  Tusoma Yn. 1:29;  Mt. 10:28;  Rum. 5:11;  Ebr. 10:3-14.  Sasa Je, Nani ni mwongo hapa, Mungu au Mashahidi?

4. Wanadai mwili wa Yesu haukufufuliwa.  Yesu alisema kwamba atafufuka, Yn. 2:19-22 na pia alionyesha mwili wake (uliofufuliwa) kwa Tomaso, Yn. 20:24-28.

5. Wanadai mwanadamu Kristo alikufa asiwe hai tena.  Lakini Biblia inasema katika Zab. 16:10, hapa Daudi alitabiriwa kuwa Yesu atafufuka.  Na Petro alidai kwamba Kristo alifufuka, Mdo. 2:30-31, wakati alipokuwa anahubiri siku ya Pentikoste alikuwa anaongozwa na Roho Mtakatifu.  Na katika Mdo. 1:1-3, Yesu alithilibitisha sana kwamba alikuwa hai.

6. Pia Mashahidi wanadai Yesu hakuwa na hali ya kimungu isipokuwa **baada ya** kufufuliwa.  Katika Yoh. 1:1-3;  17:5 tunaona Yesu alikuwa Mungu tangu mwanzo.  Katika Flp. 2:6, Yesu alikuwa sawa na Mungu, na Kristo na Mungu ni kitu kimoja, Yn. 14:11;  17:21.

Kwa hiyo wanasema kuwa Kristo aliyekufa na yule aliyefufuliwa sio mtu yule yule, wale ni watu wawili tofauti.  Lakini Biblia inasema ni yule yule kabla ya kufufuka na baada ya kufufuliwa, Mdo. 1:11;  Efe. 4:10;  Ebr. 10:12.

7. Mwisho wanadai Yesu siye mpatanishi wetu. Tusoma gazeti lao, "Watch Tower" Toleo 15/9/1909, uk. 283. "Katika toleo letu la 1906, ukarasa wa 26, tulisema, 'Bwana wetu Yesu, kati ya Baba na nyumba ya waaminio, katika kipindi cha Injili.' Usemi huu si kweli. Hakuna maandishi yanayosema hivyo. Ni sehemu ya mwisho ya kipindi cha giza, ambao tunafurahi kuufuta kutoka machaoni mwetu."

Mashahidi ni waalimu gani? Wanaobadili mafundisho yao? Nani anaweza kuamini wameongozwa na Mungu ikiwa wanasema wenyewe kuwa wamekosa katika kufundisha kwao? Lakini, ukweli ni kwamba **Yesu ndiye mpatanishi wetu**, 1 Tim. 2:5; Ebr. 9:15; 1 Yoh. 2:1.

**Mafundisho ya Mashahidi**:

***VII.*** *Nafasi ya Pili Kuokolewa.*

Kitabu chao cha "Studies in the Scriptures" Vol. 1, uk. 150, wanasema, "Ile 'fidia kwa watu wote' aliyoitoa yule 'mwanadamu Kristo Yesu' haitoi wala kuthibitisha uzima wa milele wala baraka kwa mtu ye yote; bali inamthibitishia kila mtu nafasi nyingine au jaribu la kupata uzima wa milele." Katika uk. 143, wanasema, "Nafasi ya pili itakuwa bora kuliko nafasi ya kwanza kwa sababu ya mazoezi yaliyopatikana katika matokeo ya jaribu la kwanza." Tena, katika uk. 130, 131 wamesema: "Wote walihukumiwa mauti kwa sababu ya kuasi kwake Adamu, na wote watafurahia (katika maisha hayo au yanayokuja) na nafasi kamili kupata uzima wa milele kwa masharti mema ya Agano Jipya."

**Mafundisho ya Biblia:**

**HAKUNA NAFASI YA PILI KUOKOLEWA!!!!!**

Soma Ebr. 9:27, "Kufa mara moja na **baada ya kufa hukumu."**

Lk. 9:59-60, "Akamwambia Waache wafu wawazike wafu wao."

Mdo. 13:44-46 "Kwa kuwa mnalisukumia mbali, na kujiona nafsi zenu kuwa hamkustahili uzima wa milele." Je, alisema hapa kwamba wata pata nafasi ya pili! Hata siku moja!

Ebr. 10:26, "......haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi."

Kwa hiyo tumeona kwa urahisi kwamba Biblia inatufundisha kwamba tutaishi na tutakufa mara moja tu na bada ya kufa hukumu!!

Mafundisho ya Mashahidi:

***VIII.*** *Mashahidi wanasema kuwa Chakula cha Bwana kimechukuwa nafasi ya Pasaka, na kwa hiyo, kitolewe mara moja tu kwa mwaka.*

Mafundisho ya Biblia:

Kwanza, "Usipoula mwili wake Mwana wa Adamu na kuinywa damu yake, hamna uzima ndani yenu."

Yn. 6:53-56.

Pili, Katika Biblia Wakristo hawakushiriki chakula cha Bwana mara moja kwa mwaka. La! bali Wakristo walikuwa wakikusanyika katika jina la Yesu kila siku ya kwanza ya juma (Jumapili) ili wale chakula cha Bwana. Mdo. 20:7, 1 Kor. 11:23-26, 33. Nasi tumeambiwa tufanye hivyo mpaka atakapokuja, 1 Kor. 11:26.

**Mafundisho ya Mashahidi:**

***IX***. *Ukombozi uliaanza mwaka wa 1874.*

Katika "Studies in the Scriptures" Vol. II, uk. 170. Wanasema: "1874 ilikuwa tarehe sahihi kwa kuanzisha wakati wa ukombozi na kwa hiyo kurudi kwa Bwana wetu." Katika uk. 234 wakasema, "Na kwa hivyo twaona kuwa kufufuliwa kwao (mitume) kumekwisha kutokea, na kwa hiyo wao pamoja na Bwana wapo sasa duniani, kwa kuwa hatuwaoni si tatizo kwa imani tunapokumbuka kuwa, kama alivyo Bwana wao, (mitume) nao ni nafsi ya roho, na, kama Yeye, hawaonekani kwa wanadamu."

**Mafundisho ya Biblia:**

1. Hakuna ajuaye siku ya kurudi kwa Bwana, Mk. 13:32.
2. Atakaporudi Yesu, Wakristo waliokufa watafufuliwa na Wakristo walio hai watanyakuliwa katika mawingu, 1 Thes. 4:13-17.

Ikiwa mafundisho yao ni kweli, basi wao wenyewe wamekosa wokovu, maana walikuwa bado duniani wakiandika vitabu vyao baada ya mwaka ule kupita! Mbona Biblia imeandika kwamba waamini ambao wapo ulimwenguni watanyakuliwa katika mawingu. Naona Mashahidi wamekosa kwenda Mbinguni. Na kweli walimu wote wapotofu watakosa, Gal. 1:6-9.

**Mafundisho ya Mashahidi:**

***X.*** *Wanadai "mavuno" ya injili yamekwisha!*

Katika kitabu chao, "Studies in the Scriptures," Vol 2, uk. 245, Mashahidi walisema: "Miaka arobaini ya mavuno ya kipindi cha Injili itakoma Oktoba 1914, na vivyo hivyo, upenduzi wa Ukristo, kama unavyoitwa, lazima tutegemee kuuona mara." Hivyo wanasema kuwa hakuna mtu awezaye kuokolewa baada ya Oktoba 1914, BK. Tena, Ukristo (maana yake madhebehu yote isipokuwa kanisa lao) utapinduliwa mara baada ya mwake ule.

**Mafundisho ya Biblia:**

**Mwaka 1914 umekwisha kupita zamani; mbona madhehebu bado yapo?** Isitoshe, ikiwa mavuno ya kipindi cha Injili yalikwisha mwaka 1914, basi Mashahidi wenyewe walio hai leo wamechelewa! Imekuwaje wao kudai kuwa wamejua tareje na majira hali Yesu amesema hakuna ajuaye mambo hayo? (Mk. 13:32; Mdo. 1:7).

**Mafundisho ya Mashahidi:**

***XI.*** *Roho Mtakatifu si nafsi mmoja ya Mungu bali ni nguvu fulani au himizo fulani.*

**Mafundisho ya Biblia:**

Katika Mt. 3:16, 17;  28:19 tunaona kwamba Roho Mtakatifu ni nafsi mmoja wapo ya nafsi tatu ya Uungu.

Tena katika Mdo. 5:3-4 tunaona ya kuwa Roho anaitwakuwa ni Mungu.

Lakini wakati Biblia inatufundisha ya kuwa Roho ni nafsi ni kwa sababu Roho Mtakatifu ana sifa za nafsi. Kwa mfano, kama una mnyama nyumbani, ana miguu miine, mkia mfupi, pembe mbili ndogo, chini ya mdomo ana ndevu, sasa huyu mnyama ni aina gani?  Sasa huyu mnyama ni mbuzi kwa sababu ana sifa za Mbuzi.  Lakini kama mnyama huyu ana miguu minne, mkia mrefu, ana piga kelele wakati mgeni akifika, ni mkali sana, hapendi paka, hawezi kusema kwamba huyu mnyama ni mbuzi!  Kwa sababu sifa zake sio za mbuzi
wala anasifa ya Mbwa.

Roho Mtakatifu ni nafsi kwa sababu:

Anaumiza-Isa. 63:10.
Anaweza kufundisha-Yn. 14:26.
Anaweza kusema-Mdo. 8:20.
Anaweza kushuhudia-Yn 15:26.
Anaongea yale aliyosikia-Yn. 16:13.
Aliweza kuchagua mahali pa kufanya kazi-Mdo. 13:2; 16:6-10.
Aliweza kuwapeleka wahubiri- Mdo. 13:2; 16:6-10.

**Tabia hizi zote ni za nafsi hai**.  Kama wewe unaweza kufundisha, kusema, kushuhudia, chagua mahali pa kufanya kazi, na kutuma wahubiri;  Je! ina maana wewe sio nafsi?  Kwa sababu kila mmoja hapa anauwezo huu.

**Mafundisho ya Mashahidi:**

***XII.*** *Wanadamu hawafi kwa dhambi zao wenyewe bali kwa dhambi ya Adamu.*

**Mafundisho ya Biblia:**

Katika Eze. 18:20, "**Roho itendayo dhambi, ndiyo itakayokufa**;  mwana hatauchukua uovu wa baba yake, wala baba hatauchakua uovu wa mwanawe, haki yake mwenye haki itakuwa juu yake, na uovu wake mwenye uovu utakuwa juu yake."  Imeandikwa ya kuwa **Roho itendayo dhambi, itakufa**!!  **Kumbe!!!!** Rumi 5:12, unaweza kusoma na kuona mauti iliingia ulimwenguni kwa sababu ya dhambi ya Adamu! Lakini kila mtu anakufa kwa sababu ya udhaifu wake!  Rum. 3:23, "Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa utukufu wa Mungu."  Kwa hiyo tunakufa kwa ajili ya dhambi zetu wenyewe.  Soma Rum 9:11, "Kwa maana kabla hawajazaliwa wale watoto, wala hawajatenda neno jema wala baya...."

**Mafundisho ya Mashahidi:**

***XIII.*** *Mashahidi wanafundisha kuwa si nia ya Mungu kuwaokoa watu katika kipindi cha Injili, bali ulimwengu utaokolewa katika kipindi cha utawala wa miaka 1000.*

**Mafundisho ya Biblia:**

Yesu mwenyewe alifundisha katika Mk. 16:15-16, kwamba tuhubiri Injili ili watu **waokolewe.** Na tangu siku ya Pentekoste wakovu umehubiriwa, Mdo. 2:38, 40; 13:26, 47. Pia Paulo alisema, "LEO NI SIKU YA WOKOVU", katika 2 Kor. 6:2; Fil. 2:12. Na katika Ebr. 2:3-4, mwandishi anatuambia kwa urahisi <u>kama tunakataa wokovu hatuwezi kukwepa adhabu!!!</u> Kwa hiyo ina maana tunaweza kukosa wokovu leo! Na tunakosa kwa kutotii injili, katika kipindi cha Injili.

**Mafundisho ya Mashahidi:**

***XIV.*** *Wanafundisho msalaba ni alama ya kipagani.*

**Mafundisho ya Biblia:**

Kwa kweli msalaba ulikuwa mfumo wa kutisha wa mauaji ya kikatili. Ulikuwa kwa ajili ya kuua kwa njia ya maumivu ya hali ya juu, na pia ulikuwa kwa ajili ya kutundikia mwili kama fundisho kwa watu waliowezakuuona, ambao wakati fulani uliachwa ukining'inia kwa siku kadhaa. Na tena watu wengine walitumia msalaba katika ibada ya sanamu. Ndiyo, ulikuwa wa kipagani, lakini Yesu alipopigiliwa katika msalaba wa Kirumi, maana ya msalaba ikabadilika milele.

Biblia insema kuhusu Yesu, "Ile kwa neema ya Mungu aionje mauti kwa ajili ya kila mtu," Ebr. 2:9. "Hivyo Yesu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea," Hiyo ina maana alihiari kwenda msalabani. Mtume Pualo alisema kwa Warumi, "Wote wametenda dhambi na kupuingukiwa na utukufu wa Mungu; kwa kupata haki bure kwa neema yake kwa njia ya ukombozi ulio katika ya Yesu Kristo: ambaye Mungu amekwisha kumweka awe upatanisho kwa njia ya imani katika damu yake," Rum. 3:23-25. Kwa sababu msalaba ulitumika kama njia ya Sadaka kwa ajili ya dhambi zetu, msalaba una maana kamili. "Lakini mimi, hasha, nisione fahari juu ya kitu cho chote **ila msalaba** wa Bwana wetu Yesu Kristo ambao kwa huo ulimwengu umesulibishwa kwangu, na mimi kwa ulimwengu," Gal. 6:14. Kwa watu wengi wazo la msalaba wa kikatili kuwa alama ya wokovu wetu ni upuzi. Lakini Mungu alifahamu hilo, "**Neno la msalaba,** <u>kwao wanapotea ni upuzi,</u> lakini **kwetu (Wakristo) tunaookolewa ni nguvu ya Mungu.....**tunamhubiri Kristo, aliyesulibiwa; kwa Wayahudi ni Kikwazo, na kwa Wayunani ni upuzi; bali wa waitwao Wayahudi kwa Wayunani ni Kristo, Nguvu ya Mungu na hekima ya Mungu," 1 Kor. 1:18-24. Yesu alipokwenda msalabani na kufa pale ilikuwa ni kufanya amani na Mungu kwa ajili yetu, kutupatanisha na Mungu. "Kwa kuwa katika yeye ilimpendeza utimilifu wote ukae; na kwa yeye ilimpendeza utimilifu wote ukae; na kwa yeye kavipatanisha vitu vyote na nafsi yake akiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wake," Kol.1:19-20.

Ndiyo, kuna wengi wanaoukana msalaba, wakijihesabu kuwa ni upuzi na ni wa kipagani. Lakini kwa waaminifu msalaba ni njia ya neema ya Mungu ilipanuliwa mpaka kwetu ili kuleta wokovu. "Tunatukuza msalaba" kwa sababu ni alama ya upendo wa Mungu kwetu na wokovu wetu kwa damu ya Kristo. Tena Paulo kupitia Roho Mtakatifu alisema, "Tunatukuza msalaba." Basi, kama Paulo alifundisha kupitia Roho, Tutukuzwe msalaba! Ameni!

**Mafundisho ya Mashahidi:**

***XV.*** *Tunaokolewa kwa imani tu! Wanaamini kwamba tunaokolewa kwa njia ya imani tu. Hata ingawa wanahimiza ubatizo, lakini wanasisitiza kuwa hatuokolewi kwa matendo (Efe. 2:8-9). Hivyo wanatia shaka umuhimu wa ubatizo.*

**Mafundisho ya Biblia:**

Tumeona ya kuwa (uku. 15-17) Mashahidi hawaamini ya kuwa mwili wa Yesu umefufuka. Kwa hiyo tukiangalia Rum. 6:3-4, kupita ubatizo tunatakiwa kufuata mfano wake wa kuzikwa na kufufuka. Sasa "kama" mwili wa Yesu haukufufuka, na tunajua ni lazima kwetu tuige mfano wake. Kwa hiyo kupitaia ubatizo ni lazima tuzikwe na tusifufuke kwa sababu wanadai Yesu hakufufuka.

Katika Efe. 2:8-9, Paulo anafundisha kwamba hatuokolewi kwa matendo. Lakini angalia mazingira ya mistari ya nane na tisa! Mashahidi wanashindwa kuelewa hapa kwa sababu wanakataa kusoma mazingira ya mistari hii! Soma mstari wa kwanza hadi ishirini na mbili. Paulo hapa anaongea kuhusu tofauti ya Agano la Kale na Agano Jipya!

Mst. 2, "Mlizitendea zamani." Ni lini?
Mst. 3, "Katika tamaa ya miili yetu." Ni lini?
Mst. 11, "Kumbukeni ya kwamba zamani." Ni lini?
Mst. 12, "Kwamba zamani zile mlikuwa **hamna Kristo**." Ni lini?

Sasa katika mstari wa tisa Paulo alisema, "Si kwa matendo!"
Anaongea ya kuwa leo hatutaokoka kwa matendo ya zamani kabla Kristo hajafika bado. "Matendo ya Zamani" ni Matendo ya Torati. Na ni kweli kabisa hatuokolewi kwa matendo ya Torati! Hapa Paulo anaongea kuhusu tofauti ya Agano la Kale na Agano Jipya!

Ndiyo maana katika mistari:

13, Alisema, "Lakini sasa katika Yesu Kristo."
14, "Kwa maana yeye ni amani yetu, aliyetufanya sisi sote tuliokuwa wawili kuwa mmoja; akibomoa kiambaza cha kati kilichotutenga."
15, "Naye akiisha kuuondoa ule uadui kwa mwili wake!!"

Kwa hiyo kweli hatutaokoa kwa matendo (Torati), kwa sababu YEsu alibomoa na aliondoa uadui! Matendo katika mstari wa tisa inahusu Torati (Agano la Kale, Amri Kumi). Ndiyo maana leo ni lazima tusome mazingira yote ya Biblia. Sio kuchagua mistari katika hadithi na kujenga imani juu ya mistari fulani bila mazingira ya mistari yote!

Sasa tusome Yakobo 2:14, 17 na 26. "Ndugu zangu, yafaa nini, mtu akisema ya kwamba anayo imani, lakini hana matendo: Je! ile imani yaweza kumwokoa?...Vivyo hivyo na imani, isipokuwa ina matendo, imekufa nafsini mwake....Maana kama vile mwili pasipo roho umekufa, vivyo hivyo na imani pasipo matendo imekufa."

# Sura Ya Nne

## Agano la Kale

**Mistari wanayotumia Mashahidi ili wafundishe mafundisho yao. Na mistari hiyo tunaweza kutumia ili kufundisha Mashahidi vizuri.**

**Mwanzo 1:1-2.**

Mashahidi wanatumia mistari hii ili wavamie imani ya Wakristo kuhusu nafsi ya Roho Mtakatifu. Katika mstari wa pili iliandikwa kuhusu Roho wa Mungu. Sasa mashahidi wanafundisha kwamba Roho wa Mungu ni nguvu fulani sio nafsi. Kwa hiyo watajaribu kutumia mstari huu ili wafundishe Roho ya Mungu sio nafsi lakini nguvu ya Mungu. Hata kwenye tafsiri yao ya Biblia (New World Translation of the Holy Scriptures) wametoa jina "Roho ya Mungu" na waliweka maneno mengine.

Lakini tunaweza kwa urahisi kuthibitisha kwenye maandiko kwamba Roho ya Mungu ni nafsi. Anaongea-Mdo. 13:2; anashuhudia-Yn. 15:26; anasikia-Yn. 16:13; anasikia maumivu-Isa. 63:10.

Na kwa mafundisho zaidi juu ya Roho Mtakatifu angalia Yn. 16:13; Mdo. 5:3-4; Rum. 8:26-27; na 1 Kor. 6:19.

**Mwanzo 9:4; Wal. 7:26-27; Mdo. 15:28-29.**

Mashahidi wanatumia mistari hii ili wasichukue damu kutoka kwa mtu mwingine. Na wanafundisha kuchukua damu kutoka kwa mtu mwingine ni dhambi kwa sababu haturuhusiwi kula damu.

Kwanza wanafundisha kupewa damu kutoka kwa mtu ni sawa na kula. Hapa sio kweli, wakati tunakula leo tunaweka vyakula kwenye mdomo. Hatuingizi vyakula kwenye mkono au sehemu nyingine ya mwili. Lakini tukiangali kwa makini mistari hiyo tunaona mengi.

Pili, katika Mwa. 9:4 tunaona Mungu alisema, "Bali, nyama pamoja na uhahi, yaani, damu yake; msile." Hapa Mungu anaongea kuhusu kula nyama ambayo haijapikwa au kukaushwa bado. Haongei kuhusu kutibiwa.

Tatu, Law. 7:26-27, hapa katika mistari hii miwili, Musa kweli anaongea kwa Waisraeli wasile damu. Lakini ukisoma kwa makini Law. 3:17, Musa aliwaambia Waisraeli wasile mafuta na damu. Sasa kwa nini Mashahidi wanafuata sehemu tu ya amri. Inaonekana wanachagua mafundisho yao lakini mengine wanaacha tu. Hata, hivyo Musa alitoa zile amri kwa Waisraeli chini ya Agano la Kale. Tukisoma katika 2 Kor. sura nzima utaona kufuata Agano la Kale haisaidii cho chote leo. Na tena katika Law. 7, Musa anaongea hasa kuhusu matoleo ya Waisraeli na vyakula vyao hakua na aongea kuhusu kutibiwa. Kula chakula na kutibiwa ni vitu viwili tofauti.

Nne, Katika Mdo. 15:28-29. Pia Mashahidi wanatumia hapa ili wajaribu kufundisha kwamba ni dhambi kula damu, kwa hiyo ni dhambi kuchukua damu ya mtu. Lakini katika mistari hii miwili tunaona mambo matatu. Kwanza, wasile nyama zilizotolewa kwa sanamu. Pili, wasile damu. Tatu, wasifanye uasherati (uzinzi). Sasa, kanisa la karne la kwanza waliona haya kama ni sheria ya milele. Hapana! Kwa kweli

uasherati na uzinzi ni dhambi kutoka mwanzo mpaka siku ya mwisho.  Lakini je, kula nyama au damu zile zitolewazo kwa sanamu ni dhambi mpaka sasa?  Hakuna mahali pengine kwenye Agano Jipya baada ya hapa inaonyesha tusile damu na nyama zilizotolewa kwa sanamu.  Lakini amri ya kukataza uasherati au uzinzi iko kila mahali.  Tena katika 1 Kor. 8:1-13, Wakristo walikuwa uhuru kula **vitu vyote** vilitolewa kwa sanamu.  Kama wanaweza kula na dhamili safi.  Sasa hakuna mahali pengine penye Agano Jipya inaeleza tusile vitu vilitolewa kwa sanamu!  Hata hivyo, labda sheria hii ipo mpaka sasa, lakini ilisema tusile damu.  Hakusema tusitumie damu kwa matibabu.

Tano, Mashahidi wanajulikana sana kama watu wanaoweka sheria kuhusu matibabu na kutoa badaye.  Tunajua neno la Mungu ni la Milele.  Lakini Mashahidi wanaweka sheria leo na kesho wanatoa.  Sasa Je!  Maneno ya Mungu ni ya milele au kwa muda tu?  Maneno ya Mungu ni ya milele na tena hayabadiriki, 1 Pet. 1:23-25.  Katika mwaka wa 1944 Mashahidi waliaanza kufundisha kwamba wasichukue damu ya mtu kwa kumimina.  Sasa je, mbona mwanzilishi wa Mashahidi hakujua hayo?  Mbona watu waliishi hapa kama miaka 2000 chini ya Yesu bila kujua?  Walipataje habari hiyo?  Ebr. 1:1-3 inasema Mungu anaongea kwa sisi leo kupitia mwanae.  Lakini leo Watch Tower wanafanya kama haya ni Yesu.

Sita, Katika mwaka wa 1931 mashahidi walifundisha katika kitabu chao The Golden Age, 2/4/31, uka. 293, "Kuchanjia ndui, moja kwa moja ni kinyume na agano la milele lililofanywa na Bwana." Lakini katika mwaka wa 1952 walibadirisha sheria hii, wanasema toka mwaka 1952 kwamba si sahihi kuchanjia ndui.  Mbona walisema sio sahihi, mbona walisema utavunja Aganol la Milele ukipata dawa ya kuchanjia.  Lakini sasa?

Saba, Katika mwaka wa 1967, Watch Tower waliaanza kufundisha kwamba kuhamisha kiungo cha mwili ni dhambi, soma Watch Tower 15/11/1967 uka. 702-704.  Lakini katika mwaka wa 1980, Watch Tower kwenye toleo la 15/3/1980 uka. 31, walibadirisha mafundisho yao.  Sasa hi heri tu kwa mashahidi wahamishe viungo vya mwili.

Nane, Mashahidi wanadai ni dhambi kuchukua damu ya mtu mwingine na kuiginza katika miili yao.  Lakini wapo tayari kuchukua moyo, maini, mapafu, na viungo vingine na kuingiza katika mwili wao.  Hii ni kazi ya unafiki!  Wanadai damu ni uhai, sasa moyo sio uhai?  Unaweza kuishi bila moyo?  Lakini wapo tayari kuchukua moyo wa mtu na kuingiza kwenye mwili wao kama wanahitaji.  Tena kama wakotayari kuhamisha kiungo cha mwili, huwezi kuhamisha kiungo cha mwili bila kuhamisha damu ya yule mtu waliotoa kile kiungo.

Tisa, Mbona wanabadirisha mafundisho yao, kama neno la Mungu ni la milele na halibadiriki, basi kwa nini wanabadirisha kila mara?  Mashahidi wanalaumu sana Papa (Raisi ya Katoliki) kwa sababu ana badirisha mafundisho kila mara.  Sasa kuna tofauti gani kati ya Papa na Raisi wa Mashahidi?  Hakuna hata kidogo!  Kwa hiyo subili tu, baada ya muda wata badirisha fundisho la damu kama walivyofanya mara nyingi tu!

**Mwanzo 18:1-2**

Mashahidi wanafundisha haiwezikani kwa Mungu awe na nafsi tatu.  Lakini tukiangalia sura ya 18 na 19 hapa tunaona inawezekana.  Kwanza Ibrahimu aliona wanaume (malaika) watatu.  Ibrahimu aliwaita hawa Bwana katika mst. wa 3.  Wakati wale watatu wanaongea katika mst. 9 Biblia inasema, "Wakamwambia" ina maana wote watatu wakati moja.  Mst. wa 13 tena inasema "Bwana akamwambia".  Na tunaona katika

hadithi hapa kwamba wawili wakaondoka na walienda kwa Lutu. Sasa Lutu aliwaita wale wawili Bwana (19:18) na wakati Ibrahimu alikua na ongea na Bwana bado alikuwa anamwita huyu Bwana. Wakati huu Lutu alikuwa na ongea na Bwana. Kwa hiyo tunaona kwamba ni rahisi kwa Mungu awe na nafsi tatu.

Kwa hiyo mstari huu unaweza kusaidia wewe wakati unafundisha wale. Kwa msaada zaidi angalia, Isa. 9:6; Yoh. 1:1; Yoh. 16:13; 1 Kor. 6:19; 1 Kor. 8:6; Kol. 2:9 na Ufu. 1:7-8.

**Mwanzo 40:20-22; Matt. 14:6; Marko 6:21.**

Mashahidi wanatumia mistari ya juu iliwathibitishe ya kuwa ni dhambi kushelekea sikukuu ya kuzaliwa. Kwa sababu kwenye maandiko kila mara mtu akiwa ana shika sikukuu ya kuzaliwa waliua mtu. Hapa katika Mwanzo Farao akaua mtu na Herodi wa Galilii pia akaua Yohana Mbatizaji katika sikukuu ya kuzaliwa kwake. Wanadai kwasabau hakuna mtu wa imani alikua ana shika sikukuu ya kuzaliwa basi hii ni sikukuu ya wapagani kwa hiyo ni dhambi kama sisi tunashiriki.

Kwanza, hakuna mahali kwenye maandiko inaeleza ni dhambi kusherekea sikukuu hii. Pia kama ni dhambi kuhesabu maisha yetu, kwa nini Mungu alikuwa na hesabu maisha ya watu? Soma Mwanzo 5. Mungu alikua ana hesabu watu walikuwa wanaishi miaka mingapi kwa nini sisi hatuwezi? Tena kwa nini alikuwa na hesabu maisha ya Yesu? Lk. 2:42, 3:23.

Pili, Hata hivyo wakati wanafundisha Farao na Herodi tu walishika sikukuu yao na hakuna mtu mwenye imani alishika, haya sio kweli. Soma Ayubu 1:4-5. Hapa inaeleza kwa rahisi kwamba Ayubu na watoto wake walikuwa wana sherekea sikukuu yao. Kwa ufafanuzi zaidi soma Ayubu 3:1-3.

Wanadai kwa sababu watu wawili walifanya uovu katika sikukuu zao sisi hatuwezi sikukuu zetu. Haya ni mafundisho hayamo katika maandiko.

**Kutoka 3:14**

Aangalia “Mafundisho Kuhusu Yesu” uku. 12-17.

**Kutoka 3:15**

Angalia “Kulisifu Jina La Mungu” uku. 5-6.

**Kumbukumbu la Torati 18:20-22**

Watch Tower wanadai “Nabii” hapa sio mtu mmoja lakini ni kusanyiko la watu. Na leo wanaitwa “Mashahidi wa Yehova” (Watch Tower 1/4/72, uka. 197). Kwa hiyo wanadai hawa ni huyu “Nabii”. Lakini je! Haya wanadai ni kweli au sio kweli. Tunaweza kujua kwa urahisi ina ongea kuhusu nani. Kwa sababu huyu nabii ataongea kweli soma mstari wa 22. Kwa hiyo tunaweza kupima mafundisho yao na matendo yao na tutajua kwa hakika kama hawa wanaongea kama Mungu anavyoongea. Kwa sababu Mungu sio mwongo wala sio Mungu wa michafuko. Na tunaona hapa kwenye mistari ya 20-22 kwamba huyo nabii ataongea katika jina la Yehova. Na ilitujue kama huyu “Nabii” ni kweli atathibitisha kupitia unabii wake.

Kwanza walifundisha Charles Taze Russell, alikuwa na uvuvio sawa na Biblia (Kitabu cha Thy Kingdom Come, toleo la 1903 uka. 362). Kwa hiyo huyu mtu ambaye wanadai alikuwa na pumzi ya Mungu alitabiri Vita vya Mageddon vitamaliza katika mwaka wa 1914, na Yesu atatupa mbali serikali zote ulimwenguni (utabiri huu angalia kitabu chao cha Time Is At Hand, toleo la 1904, uk. 101). Inaleweka kabisa kwa sisi wote tunaoishi leo kwamba Yesu hakurudi katika mwaka wa 1914. Leo tunatawaliwa na Mkapa, Mkapa sio Yesu Kristo!

Bado Mashahidi walitaka kutabiri, kwa hiyo katika mwaka wa 1920 waliandika, "Watafufua kama watu kamili na watu kuwa watoto wa wafalme na viongozi ulimwenguni, kufuatana na ahadi yake (Mungu)........Kwa hiyo tunaweza kujua kwa hakika kwamba wata rudi katika mwaka wa 1925, tutaona Ibrahimu, Isaaka, Yakobo na manabii waaminifu wa zamani." (Kitabu cha Watch Tower Millions Now Living Will Never Die, toleo la 1920, uka. 89-90. Je! Umewahi kusikia kwamba Ibrahimu, Isaaka na manabii wengine wanatawala siku hizi hapa uliwenguni? Hawakufika! Hawapo! Mambo yale hayakutokea!

Tena katika mwaka wa 1968 walitabiri tena Vita vya Margeddon katika mwaka wa 1975. Lakini je! Umeona? Mimi sijaona. Kwa hiyo utabiri huu kama zile za juu haukutokea!

Sasa turudi katika Kumb. 18:20-22, kama mtu anashindwa kuthibitisha maneno yake basi huyo sio wa Mungu. Kwa hiyo bwana Charles Taze Russell hakua "Nabii" kwa sababu mafundisho yake yanathibitisha ya kuwa yeye ni mwongo. Na mashahidi wote wanadai huyu ni "Nabii" katika mistari hii wanajidanganya wenyewe.

Huyu nabii ni nani? Katika mstari wa 15 hapa tunaona Musa anasema sikiliza yeye ambaye Mungu atamtuma. Sasa soma hitimisho la unabii huu katika Mdo. 3:20-26. Yule "Nabii" ni Yesu Kristo Mwana wa Mungu!

**Zaburi 37:9, 11, 29**

Mara nyingi unapoanza kuongea na Mashahidi watafungua Biblia yao hapa. Kwa sababu wanataka kuthibitisha tutarithi hapa ulimwenguni. Na hatuna tumaini la kwenda mbinguni. Kwa sababu kufuatana na Chama Cha Watchtower Mungu alifunga milango ya kwenda mbinguni katika mwaka wa 1935. Kwa hiyo ule "Mkutano Mkubwa" utarithi hapa ulimwenguni, kama watapona vita vya Megedon.

Lakini tukisoma sura hii katika mazingira yake tunaona Daudi anaongea kuhusu jinsi waovu wanavyotajirika hapa ulimwenguni. Na iwapo kama wana wa Israeli wataendelea na kumtii Mungu watarithi au kubaki kwenye nchi yao. Mara nyingi Mashahidi wanatudai hapa kuwa Daudi anaongea kuhusu mwisho wa dunia. Lakini kufuatana na mazingira Daudi anaongea kuhusu mambo yaliyokuwa na yanatokea katika maisha yake pia. Katika mst. wa 25, Daudi alikuwa anaeleza kuwa hajawahi kuona mwaminifu anakufa na njaa. Daudi alikuwa anaongea kuhusu matokeo ya mambo katika maisha yake. Sio kuhusu mambo ya baadae. Tena katika mst. wa 37, Daudi alimwambia watu waangalie mtu mkamilifu, kwa sababu katika maisha yao wataona amani. Kwa hiyo tena tunaona Daudi anaongea kuhusu mambo yaliyokuwa yana tokea katika maisha yake.

Tunajua kufuatana na kitabu cha Kum. 28, Musa alikuwa ana tabiri kuhusu matokeo ya wana Waisraeli kama wataishi maisha mazuri au mabaya. Na kwa wale ambao wataishi maisha mazuri, watarithi nchi ya

Kanaani.  Lakini kwa wale ambao wataanguka kutoka neema mbele ya macho ya Mungu basi hawa watafukuzwa mbali na Nchi ya Mungu.

Kwa hiyo kama unaongea na mshahidi kuhusu mstari huu usisahau mazingira ya sura ya 37.  Kwa sababu huwezi kuchukua mistari kutoka mazingira fulani na kuweka kwenye mazingira tofauti.  Na ukiona mstari wa kwanza na wa saba utaona kwa urahisi sura hii ina ongea kuhusu nini.

**Zaburi 110:1**

Hapa mara nyingi Mshahidi ataomba usome hapa iliajaribu kukuchanganya.  Tunaweza kuona hapa kwamba Bwana anaongea na Bwana.  Kwa hiyo mara nyingi watafungua tafsiri yao ya Biblia na kusoma na kwenye tafsiri yao inasema, "Maneno ya Yehova kwa Bwana wangu ni...."  Na kupitia tafsiri yao watafundisha vitu viwili.

1) Watadai tafsiri yao ni bora kwa sababu Bwana hawezi kuongea mwenyewe.
2) Na watafundisha Yesu aliumbwa na Yehova, kwa sababu Yehova anatoa mapendekezo yake kwa Yesu.

Kwanza, tukisoma mazingira hapa tunaona ni Baba anaongea na Yesu.  Na tunafahamu wote wawili wanajiita Bwana kwenye maandiko mara nyingi tu.  Kwa hiyo, usiache mashahid wakuchanganye wewe hapa, kwa sababu Baba anaongea na Yesu hapa.

Halafu, Je, Baba hawezi kuongea na Yesu?  Anaweza na amewahi.  Angalia katika Agano Jipya Baba aliongea na Mwana mara nyingi tu.

Pili, wanadai Yesu sio sawa na Baba kwa sababu Baba anamwambia Yesu mapendekezo yake.  Kweli, Baba anamwambia Yesu hapa atafanya nini hapa, lakini maandiko hayasemi hapa Yesu aliumbwa na Baba.  Lakini, tukumbuke mapendekezo ya Baba ni mapendekezo ya Yesu.  Kwa sababu wanania moja, kazi moja na Baba na Mwana ni Moja, Yn. 17:11.

Tena Maandiko yanatufundisha Baba ni Mungu (Yoh. 6:27) Yesu ni Mungu (Isa. 9:6; Yoh. 20:28) na kuna Mungu mmoja (1 Kor. 8:4).

Mwisho, tunajua Mungu ni nafsi tatu na anaweza kuwa katika sehemu mbali mbali wakati mmoja.  Katika Mwanzo 18:1-2, Bwana akatokea kwa Ibrahimu na katika mstari wa 2 tunaona Bwana alikuwa na nafsi, mwili, tatu.  Na katika mst. wa 3 Ibrahimu aliwaita wale watatu Bwana.  Halafu wawili walimwacha Ibrahimu na walienda Sodomu, wakati moja alibaki kwa Ibrahimu.  Na yule ambaye alibaki kwa Ibrahimu, Ibrahimu aliendelea kumwita Bwana, 18:22.  Na wakati wale wawili walifika kwa Lutu (19:1) Lutu aliwaita wale Bwana.  Wakati Bwana alimaliza kuongea na Ibrahimu yeye alirudi mbinguni.  Na Bwana kwenye nafsi mbili bado walibaki na Lutu, na Lutu aliendela na kuwaita wale wawili Bwana.  Tena katika 19:24, tunaona, "Bwana akanyesha juu ya Sodoma na juu ya Gomora kiberiti na moto toka mbinguni kwa Bwana."  Hata hapa tunaona Bwana alikuwa kwa Ibrahimu wakati Bwana alikuwa na Lutu.  Tena Bwana akafanya unyesha moto toka kwa Bwana.

Kwa hiyo kupitia hadithi hapa kwenye kitabu cha Mwanzo, ni lazima Mashahidi wakubali kuna nafsi ya Bwana zaidi ya moja.  Tena Bwana ni mmoja.  Na Bwana anaweza kufanya kazi na kuongea kwenye sehemu mbali mbali wakati mmoja tu, kwa sababu Bwana ni zaidi ya nafsi moja.  Na Bwana anaweza

kuongea na Bwana bila kushushwa chini Bwana!

**Zaburi 146:3-4**

Mashahidi wanafundisha kupitia mistari hii kwamba wakati tunakufa hakuna akili, ufahamu au ujuzi.

Lakini mwandishi alikuwa ana ongea kuhusu haya au Mashahidi wanatumia mstari mwingine bila mazingira yake. Kwa kweli wanatumia mstari mwingine bila mazingira yake.

Wazo kuu la sura ya 146 ni tunahitaji kumtegemea Mungu siyo viongozi wa ulimwengu huu. Ukisoma mstari wa 1-2 utaona wazo kuu la sura hii. Katika mstari wa 1-2 tunaona tunatakiwa kumtukuza Mungu, katika mstari wa tano tunaona Mungu ni msaada na tumaini letu inatakiwa kuwa ndani ya Mungu. Tunataka kumwamini na kumtegemea yeye kwa sababu yeye aliumba mbingu na ulimwenguni (mst. 6), analeta hukumu ya haki (mst.7), anaponya (mst. 8), anajali yatima na mjane (mst. 9), ni mfalme wa milele (mst. 10). Mwandamu lakini hawezi kutoa wokovu kwa mtu (mst. 3), kwa sababu wanadamu wote wanakufa na wakati wanadamu wanakufa kila kitu walicho kusudia kinapotea.

Kwa mfano Julius Nyerere alikuwa “Mkuu” (mst. 3). Na watu wengi walimtegemea yeye ili asaidie na kujenga maisha yao na hali ya nchi ya Tanzania. Lakini sasa kwa sababu ameshaa kufa mawazo yote aliyokuwa nazo ya kusaidia wana nchi wa Tanzania, yalitupiliwa mbali. Kwa sababu yeye hayupo sasa, watu wengine hawatafuata mawazo yake. Ndiyo maana hapa mwandishi anasema tumtegeme Mungu, yeye ni wa milele na hayewezi kufa na mawazo yake haiwezi kupotea. Kwa hiyo tumtegemee Mungu, kwa sababu tumaini la kweli, hukumu ya haki, uponyaji na wokovu uko kwenye mikono yake. Sio kwenye mikono ya “wakubwa” hapa ulimwenguni. Pia soma, 1 Kor. 2:5 na Yer. 17:5, 7.

Kwa mazumgumzo zaidi kuhusu hali ya wafu angalia Mhubiri 9:5; Ezekieli 18:4 na Luka 16:22-28.

**Mhubiri 9:5, 10**

Mstari huu inatumia mara nyingi kwa Mashahidi ili wafundishe kifo kinafuta kwa milele. Lakini tena kwa kawaida yao wanatumia mstari hii bila mazingira yake. Tunajua wazo kuu la kitabu hiki ni jinsi maisha na kila kitu cha maisha ni bure tu. Kuanzia sura ya 8:10-14 mwandishi wa kitabu hiki anaongea kuhusu mawazo ya ulimwengu kuhusu maisha, kifo, na baada ya kifo. Na anadai kwamba mtu hawezi kufanya wema uwe kiongozi wake. Kwa sababu mwandishi anadai hata ukiishi maisha mazuri sana, utakufa tu na nani atajua kama utaokoka? Anaongea haya kwa sababu anaongea kuhusu mawazo ya ulimwengu, hatuwezi kukubali na kudai mawazo ya ulimwengu ni sawa na mawazo ya Mungu.

Sasa watu wengine wata sema mbona Biblia inahusu mawazo ya Mungu tu? Hii siyo kweli, Biblia mara nyingi inaongea kuhusu mawazo ya mwanadamu hata kuhusu mawazo ya Shetani. Kitabu cha Ayubu kinahusu mawazo ya Ayubu na rafiki zake pamoja na mawazo ya Shetani (Ayu. 2:4) pamoja na mawazo ya Mungu. Kwa hiyo siyo jambo la kushangaza kwamba Mungu aliaacha mwandishi hapa aongee kuhusu maarifa ya ulimwengu. Na hitimisho la sura ya 8:10-9:10 ni kwamba, kusudi la Mungu hatuwezi kujua (8:15-17), kwa sababu hakuna maisha ya badai (9:1-10), na kwa hiyo urefu wa maisha haueleweki (9:11-16), basi mtu mwenye hekima ya ulimengu huu ataishi kwa kujipendeza mwenyewe tu! Haya ndiyo mazingira ya mistari hii.

Mistari hii siyo mafundisho ya kweli bali mafundisho ya ulimwengu huu. Mafundisho ya upagani! Sasa, kama msahidi bado anadai maneno hapa ni ya kweli na ni maarifa ya Mungu uliza yeye maswali yafuatayo:

1) Je! Unaamini watu wa Mungu ambao wamekufa watarithi mbinguni au ulimwenguni?

Watajibu ndiyo! Wanaamini wafuasi wa Mungu watarithi mbinguni na ulimwenguni. Lakini mstari wa tano una sema tena, "Wala hawana ijara tena." Maana hakuna maisha bada ya kufa kwa waliowema na wabaya. Kwa hiyo swali hili linaonyesha kwamba mawazo katika sura huu ni mawazo ya ulimwengu (wapagani).

Tena katika mstari wa 6 tunaona mwandishi anasema hawana sehemu tena. Wanani hawana sehemu tena? Wanani hawana ijara tena? Jibu liko hapa hapa kwenye mstari wa 2, "Mambo yote yawatukia wote sawasawa; kuna tukio moja kwake mwenye haki na kwake asiye haki." Kwa hiyo uliza tena:

2) Je, ukomo wako ni sawa na mtu asiyeamini?

Atajibu hapana! Lakini mstari wa pili, tano na sita inaonyesha kwamba wenye haki na wasio na haki mwisho wao ni moja! Ni tupu!

Lakini sisi Wakristo tunaelewa hapa ni mawazo ya wanadamu. Hata wanadamu wengi siku hizi wanaoamini haya. Lakini sisi kama Wakristo tunajua Yesu alienda kujiandaa mahali kwetu, Yn. 14:1-3.

**Isaya 9:6**

Mashahidi wa Yehova hawakatai hapa inaongea kuhusu Yesu. Lakini wanafundisha Yesu ni mungu moja kati ya miungu wengi (1 Kor. 8:5) vile vile Shetani ni mmoja wapo (2 Kor. 4:4). Kumbuka Mashahidi wanaona Yesu kama aliumbwa na Baba. Kwa hiyo kupitia mafundisho yao wanakataa kwamba Yeye ni Mungu mwenye nguvu zote.

Wanadai wana Mungu wenyewe nguvu zote na Mungu mwenye nguvu. Kwa hiyo wanafundisho Mungu mwenyewe nguvu zote ni Baba wakati Mungu mwenye nguvu ni Yesu. Lakini kwa kweli, wanaabudu nafsi moja tu ya Mungu, Baba.

Lakini unaweza kuwabana mashahidi kwenye njia mbili hapa rahisi tu.

1) Uliza Mshahidi kama anaamini kuna Mungu moja wa kweli? Watajibu kila mara ndiyo. Tena uliza, "Basi, huyu Mungu moja wa kweli ni nani?" Watajibu Yehova au Baba. Sasa omba wasome hapa katika Isa. 9:6, sasa uliza tena, "Huyu, Mungu mwenye nguvu ni nani?" Watakubali Yesu ni Mungu mwenye nguvu. Tena uliza, "Je, Yesu ni Mungu moja wa kweli?" Wata jibu "hapana! Yeye ni moja kati ya wengi." Kama umefika hapa umwambie kwamba mafundisho yao yanaleta hitimisho mbili. Kwanza, kama Yesu sio Mungu wa kweli basi yeye ni Mungu asiye na kweli. Au, wana Mungu wawili wa ukweli. Na tunajua kufuatanan na Biblia nzima kuna Mungu mmoja tu! Sasa, kumbusha pointi kubwa hapa, katika mstari wa 6 inasema huyu mtoto pia atajulikana na ataitwa, "Mungu mwenye nguvu na Baba wa Milele." Mbona Mashahidi wanafundisha kuna Baba mmoja tu na yeye ni Yehova lakini hapa Isaya anasema, huyu mtoto ni **Baba wa Milele**!

2) Pia unaweza kuwabana mashahidi kwa sababu wanafundisha kuna Mungu mwenye nguvu zote na Mungu mwenye nguvu na wale miungu ni tofauti.  Hapa katika Isa. 9:6 tunaona Yesu ni Mungu mwenye Nguvu.  Sasa omba wasome Isa. 10:20-21, hapa Yeremia anafundisha kwamba Watu wa Yuda watarudia kufuata Mungu mwenye nguvu.  Huyu Mungu mwenye nguvu hapa ni nani?  Ni yule aliyetoa sheria pamoja na Musa.  Na kumbe yeye pamoja na Yesu wote wawili ni wenye nguvu.  Maneno yale yale yanaongea kuhusu Mungu hapa yanatumika katika Isa. 9:6 kuhusu Yesu!

Tena katika Mat. 28:18-20, Yesu alisema amepewa mamlaka yote hapa ulimwenguni na mbinguni.  Kwa hiyo kama tunajua mtu mwenye mamlaka yote ni Mkuu.  Nani atakataa hapa?  Sasa, soma Yer. 32:18, hapa tunaona Mungu aliye Mkuu.  Mungu wa Waisraeli aliye Mkuu.  Mbona Yesu anamamlaka yote?  Mbona Mungu hapa katika Yer. 32:18, ana mamlaka yote.  Ni kwa sababu, Yesu na Baba ni wa Moja!

Tena angalia mazumgumzo katika Yn. 1:1;  Yn. 20:28 na Ufu. 1:7-8.

**Isaya 43:10**

Mashahidi wanatumia mstari huu ya kuonyesha hawa tu ni watu walichaguliwa na Mungu.  Na Mungu alipewa jina la Mashahidi kwa hawa.

Kwa kweli, mashahidi wa Yehovah hawakutumia jina lile mpaka mwaka wa 1931.  Walichagua hilo jina katika mji wa Columbus, Ohio Marekani.  Na walichagua jina lile lile kuwatenganisha hawa kutoka kwa makundi mengine ya watu ambayo walikuwa wana mfuata Charles Russell.

Na Yesu alionyesha kuwa na jina tu sio maana utapewa wokovu.  Mat. 7:21-23, "Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni.  Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi?  Ndipo nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe;  ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu."

Na kwa kutamani jina la Mungu zamani sana ya Ki-ebrania, na kuliacha jin la Yesu Kristo.  Mashahidi wa Yehova wanafanya sawa sawa na Wayahudi katika karne ya kwanza.  Tukumbuke Yesu alisema, "Mtakuwa mashahidi wangu,"  Mdo. 1:8.  Na historia inafundisha kwamba, "Na wanafunzi walijiita Wakristo,"  Mdo. 11:26.

**Ezekieli 18:4**

"Kwa hiyo roho zetu zitakufa na bada ya kufa hatutakuwa na dhamiri."  Ndiyo maneno ya Mashahidi kuhusu mstari huu.  Lakini je, haya ndiyo mawazo ya maandiko au mawazo ya Mashahidi tena.  Pole kwao ni mawazo yao tena.  Tena wamechukua mstari pasipo mazingira yake.  Mwandishi alikuwa ana ongea kuhusu nini hapa?  Watoto Waisraeli walikuwa wana lalamika kinyume na Mungu, kwa kunukulu mithali moja ya zamani, "Baba wamekula zabibu mbichi, nao watoto wakatiwa ganzi la meno?"  Wana Waisraeli walikuwa wana lalamika kwamba adhabu ya wazazi wao ilianguka juu yao.  Na mstari wa 4 ni jibu la Mungu, yule ambaye anatenda dhambi atakufa.  "Tazama, roho zote ni mali yangu;  kama vile roho ya baba ni mali yangu, ndivyo ilivyo roho ya mwana mali yangu;  roho ile itenday dhambi itakufa."  Kwa hiyo mazingira ya mistari hii ni kwamba Mungu hakuwa ana ongea kuhusu hali ya watu waliotangulia kufa.

Alikuwa ana ongea kuhusu watu waliokuwa wana ishi. Na alitumia neno “roho” kwa kusimamia mtu aliye hai. Kwa maana mtu atendaye dhambi atakufa, Rum. 6:23.

Neno “Roho” inatumika katika njia nyingi katika maandiko.
1) Inasimamia maisha ya mtu.
2) Inasimamia mtu mwenyewe (kama hapa Eze. 18:2-4).
3) Inasimamia utu wa ndani ambao unaishi kwa milele.

Mashahidi wanafundisha wakati tunakufa kimwili tunakufa moja kwa moja, dhamiri yetu haiendelei. Lakini kuna maandiko mengi yanathibitihsha ya kuwa roho ni ya milele: Lk. 12:4-5; 2 Kor. 5:1, 8-10; Ufu. 6:9-11.

**Danieli 10:13, 21; 12:1**

Chama cha Watchtower kinafundisha Mashahidi kwamba Yesu Kristo ni malaika tu, aliyezaliwa kama mtu mwingine, alikufa kwa sadaka ya dhambi na alifufuliwa kama malaika. Wanaeleza, “Yesu Kristo ambavyo tunaelewa kutoka kwenye Maandiko yeye ni Mikaeli mkuu wa mbele....” (Watchtower 15/2/79, uka. 31). Lakini Je! Biblia inafundisha haya? Au, ni fundisho la Chama Cha Watchtower linalazimisha wafuasi waamini tu?

Maandiko ya Mungu yanataja Mikaeli mara tano tu:

1) Mmoja wa hao wakuu wa mbele, Dan. 10:13.
2) Mkuu wenu [wana Waisraeli], Dan. 10:21.
3) Jemadari mkuu, asimamaye upande wa wana wa watu wako [wana Waisraeli], Dan. 12:1.
4) Malaika mkuu, aliposhindana na Shetani, Yuda 9.
5) Mikaeli na malaika zake wakapigana na yule joka, Ufu. 12:7.

Sasa ni mstari upi kati ya hii unasema Mikaeli na Yesu ni sawa, ni mtu mmoja? Ni mstari upi hapa unasema Mikaeli ni Yesu Kristo? Hakuna hata mmoja!

Tena, Mashahidi watafungua 1 Thes. 4:16, na kusoma, “Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu....” Mashahidi wanadai kwa sababu Yesu anatumia “sauti ya malaika mkuu” basi Yesu ni malaika, kwa hiyo yeye ni Mikaeli. Lakini tukiendela kusoma tunaona Yesu pia atatumia “parapanda ya Mungu”. Kwa hiyo kama Yesu ni malalika kwa sababu atatumia sauti yao, basi kufuatana na hoja yao basi Yesu ni Mungu pia kwa sababu atatumia parapanda ya Mungu. Kwa hiyo tunaweza kuona hapa jinsi wanavyobadilisha mstari huu iliwafundishe mafundisho yao. Mstari huu unafundisha kwamba Yesu atakapokuja tutasikia sauti ya Malaika na parapanda ya Mungu. Mstari huu hausemi Yesu ni malaika. Yesu atatumia sauti ya malaika.

Sasa, labda Biblia inafundisha mahali pengine kwamba Yesu ni malaika? Hapana, bali ukisoma Waraka kwa Waebrania sura ya kwanza utaona jinsi mwandishi pale alikuwa ana thibitisha kuwa Yesu ni bora kuliko malaika.

Mstari wa 5, “Kwa maana alimwambia malaika yupi wakati wo wote, Ndiye mwanangu, Mimi leo nimekuzaa? Na tena, Mimi nitakuwa kwake Baba, na yeye atakuwa kwangu Mwana?”

Mstari wa 6, “Hata tena, amletapo mzaliwa wa kwanza ulimwenguni, asema, Na wamsujudu malaika wote wa Mungu.”

Mstari wa 8, “Lakini kwa habari za Mwana asema, Kiti chako cha enzi, Mungu, ni cha milele na milele; Na fimbo ya ufalme wako ni fimbo ya adili.”

Mstari wa 10, “Na tena, Wewe, Bwana, hapo mwanzo uliitia misingi ya nchi, Na mbingu ni kazi za mikono yako.”

Tena malaika mzuri alikataa watu wasimwabudu.  Katika Ufu. 22:8-9, Yohana alitaka kuabudu malaika, na yule malaika alikataa na alisema uabudu Mungu.  Lakini katika Ebr. 1:6, Mungu aliamuru malaika wote waabudu Yesu.  Tena tunahitaji kukumbuka Yoh. 5:23, “Ili watu wote wamheshimu Mwana kama vile wanavyomheshimu Baba.”

# Sura Ya Tano

## Agano Jipya

**Mathayo 3:11**

Katika kitabu cha Watchtower, Unaweza Kuiishi Kwa Milele Katika Paridiso Ya Dunia, kilitolewa 1982, ukarasa ya 40, tunaona wameandika, “Yohana Mbatizaji alisema Yesu atabatizwa na roho mtakatifu, kama yeye alikuwa na kubatizwa na maji. Kwa hiyo kama maji siyo mtu basi roho mtakatifu siyo mtu.”

Kwa hiyo kwa sababu Roho Mtakatifu alitajwa kwenye mstari pamoja na kitu asiye hai wanadai Roho sio mtu. Sasa hii ni akili ya mtu mzima au mtu ambaye amechanganyika kidogo.

Tuaangalie Mwanzo 1:9, “Mungu akasema, Maji yaliyo chini ya mbingu na yakusanyike mahali pamoja, ili pakavu paonekane; ikawa hivyo.” Kwa sababu Mashahidi wanadai Roho Mtakatifu sio hai kwa sababu alitajwa pamoja na maji, na katika maji hakuna uhai. Basi Mungu si hai kwa sababu alitajwa pamoja na maji, na katika maji hakuna uhai.

Tena, katika Matayo 3:11, kama Roho Mtakatifu siyo kitu chenye uhai kwa sababu alitajwa na maji basi tukumbuke hata Yesu alitajwa hapa. Kwa hiyo kama Roho Mtakatifu hana uhai kwa sababu alitajwa pamoja na maji basi hata Yesu hana uhai.

Lakini ukimwuliza Mshahidi kama Mungu ana uhai au kama Yesu ana uhai, wata jibu ndiyo. Sasa inawezekana Mungu na Yesu wawe na uhai kama wametajwa na maji kama roho? Kwa urahisi tunaona hapa hali ya ujinga ya majadiliano yao. Haina maana kuwa ukitajwa na maji basi huna uhai. Tufikiri kidogo, Je! Umewai kunywa maji? Je! Unahai wakati unakunywa maji au hukuwepo. Tufikiri tena, Je! Umewai kutumia jina lako au jina la mtu fulani katika sentenci pamoja na neno “maji”? (Mfano: Mtoto anahitaji maji.) Kama umewai, Je huyu mtoto alikuwa hai? Ndugu zangu, kwa sababu Roho Mtakatifu alitajwa pamoja na “maji” haina maana hata kidogo ya kuwa Roho hana uhai.

**Mathayo 6:9**

Mashahidi wanatumia mstari huu bila utaratibu. Wanaeleza kwamba jina la Mungu linatakiwa litukuzwe, na wanadai tunatakiwa kutumia jina la “Yehova” kwa sababu ya mstari huu. Na wanasema kama hatutumia jina”Yehova” basi Mungu hawezi kusikia maombi yetu.

Je! Hapa katika Mathayo sita Yesu alikuwa ana fanya nini? Alikuwa ana fundisha wanafunzi wake jinsi ya kuomba. Na Yesu alifundisha tuanze maombi yetu kwa kusema, “Baba yetu uliye mbinguni..” Je! Yesu alisema, “Yehova uliye mbinguni?” HAPANA!

Yesu aliomba mara nyingi tu katika Agano Jipya, na tunajua kufuatana na maisha yake Yeye alikuja iliatuongoze tufike kwa Baba. Na ni wapi kwenye maandiko Yesu alikuwa ana anzaa maombi yake kwa kumwita Mungu, “Yehova”?

Katika Yoh. 11:41, “....Akainua macho yake juu, akasema BABA...” Hakusema “Yehova”. Katika Marko

14:36, "...Akasema, Aba BABA...."  Hakusema "Yehova".
Katika Yoh. 17:1, "...Akasema BABA..."  Hakusema "Yehova".

Sasa kazi ya Yesu ilikuwa kutupeleka kwa Baba, Yoh. 14:6.  Sasa alifundisha wanafunzi wake wakati anataka kuomba anazaa ombi lake kwa kusema, "Baba yetu uliye mbinguni."  Tena kwa matendo alitumia neno "Baba" na "Aba Baba."  Hakuwai kuonyesha mfano wa kuanza ombi kwa kutumia jina "Yehova". Na tunajua kama tunataka kuwa rafiki yake tutafanya kama alivyoamuru, Yoh. 14:15 na 15:14.  Pia tunahitaji kudumu katika mafundisho ya Yesu vinginevyo hatuna Mungu, 2 Yoh. 9.  Sasa, tuamini nani, maneno, mafundisho, matendo ya Yesu au maneno ya Chama ambacho wanatumia mistari ambayo haisemi kama Biblia isemavyo wanataka mstari iseme!

**Mathayo 14:6-10**

Angalia kwenye kitabu hiki, Mwanzo 40:20-22.

**Mathayo 24:3**

"Hata alipokuwa ameketi katika mlima wa Mizeituni, wanafunzi wake wakamwendea kwa faragha, wakisema, Tuambie, mambo hayo yatakuwa lini?  Nayo ni nini dalili ya kuja kwako, na ya mwisho ya dunia?"  Mstari wa 4, "Yesu akajibu, akawaambia, Angalieni, mtu asiwadanganye."

Kwa huzuni mtu ameshaa danganywa Mashahidi, na ni lazima tuangalie kwa makini au watadanganya wengine pia.  Mashahidi wanabadirisha maneno katika mstari wa 3 "kuja kwake" iwe "utakuwapo lini". Na katika tafsiri yao wametoa kabisa maneno "kuja kwako" na wameweka "utakuwapo lini".

Kwanza kabisa, tunahitaji kuagopa mtu au Chama ambacho wapo tayari kubadirisha hata neno moja la maandiko!

Pili, Wameweka neno "kuwapo" kwa sababu ya mafundisho yao yanaeleza ya kuwa Yesu alirudi kwa siri katika mwaka wa 1914 na ame- "kuwepo" tangu siku ile.  Na ame- "kuwepo" kwa kuongoza Chama Cha Watchtower!

Tatu, katika mazingira ya Mat. 24, Yesu aliendelea na kusema katika mistari wa 11, 23-26, "Na manabii wengi wa uongo watatokea, na kudanganya wengi......Wakati huo mtu akiwaambia, Tazama, Kristo ypo hapa, au yuko kule msisadiki.  Kwa maana watatokea wakristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu;  wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule.  Tazama, nimekwisha kuwaonya mbele.  Basi wakiwaambia, Yuko jangwani, msitoke; yumo nyumbani, msisadiki."

Kutokana na hayo Mashahidi wanadai Yesu "yumo nyumbani" katika Chama chao.  Na kama unataka kujua Yesu unahitaji kuwauliza wao.  Lakini kwa wazo ambalo tunaangalia sasa hakuna sababu ya kufungua Biblia ilituonyesha kwamba wamekosea hapa.  Tunaweza kuangalia kwenye vitabu vyao na kuonyesha kwamba Chama Chao ni Chama Cha Manabii ya Uongo.  [Angalia Kumb. 18:20-22].  Tena mafundisho yao yanabadirishwa kila miaka kadhaa.

Ni kitu cha kushangaza kwa sababu wanafundisha kuwa Yesu alianza kuonekana katika mwaka wa 1914. Lakini ni kitu cha kushangaza zaidi wakati unaanzaa kufundisha haya wakati ulishaa anza kufundisha

katika mwaka wa 1874 kwamba Yesu alirudi mwaka ile.  Gazeti la Watchtower ililianza kuchapwa katika mwaka wa 1879, na katika mwaka ule Watchtower iliitwa “Watchtower ya Zioni na Mjumbe wao Alijulikana Yesu”.  Na baada haya miaka 50 J. F. Rutherford aliandika kitabu, “Julikana”, na katika ukarasa wa 65, Rutherford alisema, “Uthibitisho wa maandiko ni kwamba Bwana Yesu Kristo alionekana kwa mara ya pili katika mwaka wa 1874 bk.”  Lakini sasa Chama Cha Mashahidi kinafundisha Yesu aliaanza kujulikana tena katika mwaka wa 1914.  Kwa kukiri na vitu vyao, hawa ni manabii wa uongo, Rutherford mwenyewe aliandika na kudai Yesu alijulikana kwa mara ya pili katika mwaka wa 1874 lakini sasa wanasema mwaka wa 1914.

Katika Watchtower 1/12/82, ukarasa ya 23, waliandika, “Katika karne ya kwanza, Yerusalemu ilikuwa mahali pa kutoa madaraka ya Ukristo (Mdo. 15:1-2).  Lakini leo madaraka yake yanatolewa kutoka kwa Brooklyn, New York.”  Ni wapi kwenye maandiko Yesu alisema ataanza kutoa mamlaka hapa ulimwenguni kupitia mji mchafu sana wa Brooklyn?  Hakuna mahali.  Yesu leo anatuongoza kutoka mbinguni, Mat. 28:18-20;  Yn. 14:1-3.  Tena tunahitaji kuwaogopa hawa, Kumb. 18:22.  Kwa sababu wanaongea kupitia mamlaka yao siyo kupitia mamlaka ya Yesu.   Mat. 24:30-31, tunaona kwamba kila mtu atamwona Yesu atakaporudi, siyo badhi ya watu tu.

**Mathayo 24:14**

Mstari huu ni mzuri kwa Mashahidi toka mwanzo wa dini yao.  Lakini kama kawaida wanaelewa mstari huu bila kuangalia mazingira yake.  Kama tunafahamu Mashahidi wanaaamini Yesu alirudi kwa siri katika mwaka wa 1914 bk na ali- “anzisha” ufalme wa Mungu kule mbinguni wakati huu, na alifanya Chama Cha Watchtower kiwe mjumbe wake hapa ulimwenguni.  Kwa hiyo wanadai kama unataka maisha ya milele, unahitaji “uje kwenye shirika la Yehova kwa wokovu,” The Watchtower 15/11/81, uka. 21.

Wakati wanahubiri “injili” au “habari njema” kuhusu ufalme, kwa kweli wanahubiri mafundisho yao jinsi Yesu alivyorudi kwa siri katika mwaka wa 1914 bk.  Tena, wanakubali wazi wazi kwamba”habari njema” wanayofundisha siyo ile habari njema iliyofundiswa na Wakristo kutoka karne ya kwanza mpaka sasa.  Na wanafikiri siyo kitu cha ajabu kwamba wana
injili TOFAUTI:

“......Ufalme iliyoshahidi wa Mashahidi wa Yehova kutoka mwaka 1914 ni kitu tofauti sana na kile ambacho wamisionari wa Ukristo walieneza kabla na baada ya 1914.  ‘Tofauti’ -- kubwa gani?...Maelezo Mashahidi ya Yehova wanahubiri kutoka mwaka wa 1918 ni kitu tofauti......kuhubiri habari njema ya Ufalme wa Mesia ulijengwa kule mbinguni mwaka wa 1914....”  Watchtower 1/10/80, uka. 28-29.

Lakini Biblia inatuonya kuhusu kuhubiri injili au habari njema tofauti:

“Nastaajabu kwa kuwa mnamwacha upesi hivi yeye aliyewaita katika neema ya Kristo, na kugeukia injili ya namna nyingine.  Wala si nyingine;  lakini wapo watu wawataabishao na kutaka kuingeuza injili ya Kristo.  Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, **na alaaniwe.**  Kama tulivyotangulia kusema, na sasa, nasema tena, mtu awaye yote akiwahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo mliyoipokea, na alaaniwe**,**” Gal. 1:6-9.

Mashahidi ya Yehova kupitia Gazeti lao wanafundisha injili tofauti, sasa tuwaache walaaniwa!  Ni wapi Paulo aliwaambia Wagalatia kwamba Yesu atarudi kwa siri na kuweka makao makuu yake Brooklyn, New

York katika mwaka wa 1914? Hakuwahi! Kwa hiyo ina maana wanahubiri injili nyingine, na walikubali wenyewe. Tuwaache waalaniwe!

**Mathayo 24:34**

“Amin, nawaambia, Kizazi hiki hakitapita, hata hayo yote yatakapotimia.”

Kizazi kipi? Mashahidi wanasema ni kizazi cha mwaka 1914! Kwa hiyo kufuatana na madai yao na maneno ya Yesu, “Kizazi cha 1914 hakitapita, hata hayo yote yatakapotimia.”

“Ushuhuda unaeleza kuwa kizazi cha 1914 kama kizazi kilichoongelewa na Yesu. Basi, ‘kizazi hiki haiwezekana kupita mpaka haya yote yatakapotimia,’ ” The Watchtower 15/2/86, uka. 5.

Kwa miaka mingi katika Gazeti lao “Awake” ndani ya kila toleo katika ukarasa wa pili walichapa, “Kwa muhimu zaidi, gazeti hili linajenga faraja katika ahadi ya Uumbaji kwamba amani na usalama wa Taratibu Mpya [Ulimwengu Mpya] utaingia kabla kizazi kile kilchona matokeo ya 1914 hakijapita,” Awake. Katika kitoleo ya 8/10/68, ya Awake, walifafanua zaidi kwa kusema, “Yesu bila shaka alikuwa ana ongea kuhusu wale waliokuwa na umri mkubwa wa kutosha ya kuelewa ni nini kilitokea.” kwa kudai, “vijana wa umri 15” ukarasa 13. Tena walisema vya kizazi kwa kweli hakiwezi kuwa na watoto waliozaliwa katika kipindi cha Vita Vya Dunia vya Kwanza, Watchtower, 1/10/78, uka. 31.

Mtu anahitaji kupiga hesabu na kuangali jinsi Mashahidi walivyoingiza tatizo katika mafundisho yao. Leo ni mwaka wa 2000, mashahidi wanadai kizazi kile waliokuwa na umri wa miaka 15 katika mwaka wa 1914, kwa hiyo walizaliwa katika mwaka wa 1898. Mtu ambaye alizaliwa katika mwaka wa 1898 ana miaka mingapi leo? 100 au zaidi! Kwa hiyo kizazi kile kitapita hata kesho, labda wako wachache sana sasa wanaobaki katika mwaka wa 2000. Na Mashahidi wanaogopa wataonekana tena kama manabii wa uongo walibadirisha mafundisho yao ya awali!!!! (Je, Yesu mara ngapi alibadirisha mafundisho yake, katika Biblia?) Kwa hiyo mwaka wa 1984 kwenye Watchtower 15/5 uka. 5 walichapa imani mpya yao, “Kama Yesu alitumia ‘Kizazi’ katika hali ile na tunatumia mwaka 1914, basi watoto wale wana miaka 70 tu au zaidi.” Angalia jinsi walivyobadirisha mafundisho yao, katika mwaka wa 1984 walisema kizazi kile ni watu 70 au zaidi. Inamaana sasa wanafundisha kizazi kile siyo watu waliozaliwa katika mwaka wa 1898 bali ni watu waliozaliwa katika mwaka wa 1914. Umeona jinsi walivyofanya. Walijua kwamba kile kizazi cha 1898 kilikuwa kina toka hapa uliwenguni kwa hiyo walibadirisha mafundisho yao kwa kusema hatukuelewa Yesu, WANAMLAUMU YESU kwa kosa lao! Hata hivyo tuangalie kidogo, leo ni mwaka wa 2000, watu waliozaliwa katika mwaka 1914 wana umri 85 au zaidi. Mbona kizazi kile kinafutwa sasa hivi wakati unasoma haya. Sasa Chama Cha Mashahidi watafanya nini? Naona watabadirisha mafundisha yao tena, na labda watamlaumu Yesu tena! Sijui, mimi siwezi labda wewe unaweza kumlaumu Yesu? Chama Cha Mashahidi wanafanya hivyo. Je, unataka kuwa kwenye Chama Cha watu ambao wanamlaumu Yesu? Unafiriki Yesu atafanya nini siku ya mwisho na wale watu?

**Mathayo 24:45-47**

“Ni nani basi yule mtumwa mwaminifu mwenye akili, ambaye bwana wake walimweka juu ya nyumba yake, awape watu chakula kwa wakati wake? Heri mtumwa yule, ambaye bwana wake ajapo atamkuta akifanya hivyo. Amin, nawaambieni, atamweka juu ya vitu vyake vyote.”

Mistari hii ni mistari muhimu sana kwa Chama Cha Mashahidi.  Wanadai Chama Chao in "mtumwa mwaminifu" na wanauwezo zaidi wa Biblia kutoa "chakula cha kiroho" kwa kila mtu.  Kwa kufundisho haya wanafanya wawe na mamlaka zaidi ya Biblia, ndiyo maana hata kama wanafundisha kitu ambacho ni kinyume na maandiko wafuasi wao hawajali.  Wataendelea kufuata Chama mpaka jehanum.

Watchtower, 1/12/81, uka.27, "Yehova Mungu aliweka tayari shirika la kuonekana, "mtumwa mwaminifu" wake, limejaa na watu waliokwa roho, ili wasaidie Wakristo katika nchi yote waelewa na kutumia kwa usahihi Biblia katika maisha yao."

Ukarasa 31, "Majaliwa kwa kweli ni wale wote wanaotumikia pamoja na chama cha 'mtumwa mwaminifu', mjumbe wa Yehova ambaye anajulikana."

Sasa tusome 2 Pet. 1:20-21, "Mkijua neno hili kwanza, ya kwamba hakuna unabii katika maandiko upatao kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani tu.  Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walienena yaliyotka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu"

Waebrania 1:1-2, "Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufuanya ulimwengu."

Kwa katika mistari hii ya Biblia tunaona hakuna mtu anayeweza kutafsiri Biblia kama anavyotaka na Mungu anaongea nasi leo kupitia Mwanae.  Mashahidi wa leo wanaamini haya pia lakini wanadai kuwa Yesu yupo Brooklyn, New York na anaongoza watu wao.  Lakini ukisoma habari kwenye kitabu hiki katika Mathayo 24:34, unaona kwa urahisi wanadai hata hawa hawaelewi Yesu katika kipengele fulani.  Kwa hiyo kama wamekosa kuelewa Yesu katika kipengele kimoja ni nini kitazuia wasialewe Yesu katika vipengele vingine?

**Mathayo 26:27**

Chama Cha Watchtower kinafundisha wafuasi wao wasiotii amri ya Yesu Kristo katika mistari hii.  Kwa hiyo wakati Mashahidi wanashiriki meza ya Bwana (mara moja kwa mwaka), mkate na kikombe vinapita tu bila mtu kushiriki.  Katika mwaka wa 1986, Chama kilihesabu watu walioabudu katika sikukuu yao ya Meza ya Bwana.  Watu 7,792,109 walisali na kati yao ni watu 49,716 tu walishiriki Meza ya Bwana.  Kwa hiyo ina maana watu wachache sana walishiriki Meza ya Bwana kama Yesu alivyoamuru.

Kwa kushindwa, "Nyweni nyote katika hiki," kama Yesu alivyoamuru, ni fundisho kwa Chama Cha Watchtower.  Watchtower kinafundisha kutoka mwaka wa 1935 kwamba hatuwezi kushirikiana pamoja na Yesu katika Agano Jipya, (Ebr. 12:24).  The Watchtower, 15/2/86, uka. 15 wanasema, "Wale ambao wako kwenye kundi la 'kondoo wengine' hawapo kwenye agano jipya na hawashiriki."

Lakini Yesu alisema katika Yoh. 6:53, "Basi Yesu akawambia, Amin, amin, nawaambieni, Msipoula mwili wake Mwana wa Adamu na kuinywa damu yake, hamna uzima ndani yenu."  Kwa hiyo kama Mashahidi wanakataa kula Meza ya Bwana basi wanakataa uzima wa milele.

Pia mwulize Mshahidi aonyeshe katika Biblia sehemu ambayo Yesu alisema siku ya kutumia Meza ya Bwana ni mwaka wa 1935?  Hakuna mstari wo wote!

Angalia Ufu. 7:9, kwa habari za 1935 na angalia Yoh. 10:16 kuhusu kondoo zingine.

**Marko 1:8**

Angalia mazumgumzo katika Mat. 3:11.

**Marko 6:21-25**

Angalia mazungumzo katika Mwa. 40:20-22.

**Marko 12:29**

Huu ndiyo mstari ambao Chama Cha Mashidi wanatumia vibaya kuhusu mafundisho yao yaani hakuna nafsi tatu katika Uungu. Wanasititiza sana, "Bwana wetu ni Mungu mmoja." Ambacho wanashindwa kuelewa ni kwamba Agano Jipya linafafanua Mungu mmoja ni umoja wenye sehemu, (kama nyumba ni moja wenye vyumba vingi).

Kwa kweli Wayahudi wengi hawakuelewa kwamba Mungu alikuwa na nafsi tatu. Ni kwa sababu Mungu hakuwafafanulia. Lakini kwa macho ya Mashahidi, ukweli uliofafanuliwa umefichwa kutoka macho yao kwa sababu ya viongozi wao.

Hata hivyo Biblia inafundisha kwamba kuna Mungu mmoja, hatuwezi kukataa. Pia hatuwezi kukataa kuwa Mungu ni umoja wenye sehemu. Angalia kwenye Biblia mistari hii: Mat. 3:13-17; 1 Yoh. 5:6-13.

Pia angalia mazungumzo katika kitabu hiki chini ya Mwa. 18:1-2; 1 Kor. 6:19; Kol. 2:9 na Ufu. 1:7-8.

**Luka 3:16**

Angalia mazungumzo katika kitabu cha Mat. 3:11.

**Luka 16:22-24, 27-28**

Mashahidi wa Yehova wanafundisha kwamba "kuzimu" ni kaburi na hakuna ufahamu au dhamiri kuzimu mpaka ufufuo utakapotokea. Na kwa sababu mafundisho ya Yesu hapa yanapinga mafundisho yao basi wanadai hapa ndiyo mfano tu kwa hiyo sivyo ilivyo.

Kwa tafsiri yao Watchtower inafundisha, Lazaro ni mwanafunzi wa Yesu, matajiri ni Viongozi wa Wayahudi, na Ibrahimu ni Yehova Mungu. Kwa hiyo wanadai vifo vya Lazaoro na Ibrahimu vinamaana vipindi vipya vilianzishwa baada ya vifo vyao. Na wanafundisha maumivu ya Lazaro ni kuweka wazi dhambi ya viongozi wa Wayahudi kupitia mafundisho ya Mitume. Kwa hiyo wanakataa kabisa kwamba Yesu alikuwa ana ongea kuhusu hali ya watu kama wameshafariki.

Kwa kweli hakuna hata mtu anayeweza kukataa na kusema kuwa hili hapa sio fundisho la Yesu. Tena tunaelewa ni mfano kati ya mifano mingi ya Yesu. Lakini pia tunaelewa mifano yote ya Yesu ilifafanua hadithi za kweli ambazo ziliwahi kutokea mara nyingi.

Shida ni kwamba Mashahidi wanakataa mafundisho ya kuteswa badaa ya maisha haya.  Wanakataa kwa sababu ya nyingi tu.  Lakini hata kama hatupendi ya kuwa watu watatupwa jehanum au watateswa sisi ni nani kumhukumu Mungu?  Tena sisi ni nani kupinga mafundisho ya Mungu?  Wakati Ibrahimu alisikia Mungu anataka kuagamiza Sodomo na Gomorah alisema, “Hasha;  Mhukumu ulimwengu wote asitende haki?”  Tunahitaji kuwa kama Ibrahimu, na tuelewe tu Mungu atahukumu watu na atahukumu kwa haki?  Tena tunahitaji kuelewa sisi ni viumbe wa Mungu hatuna haki ya kumlaumu yeye kwa kazi yake ya hukumu!  Na siyo hapa tu katika Luke 16, Yesu anafundisha kuhusu hukumu baada ya kufa.  Usome mistari hii:  Mat. 13:41-42;  Luka 13:27-28;  Mat. 13:49-50;  Mat. 22:13;  Mat. 24:50-51;  Luka 12:46-48; Mat. 25:30;  Mat. 26:24;  Marko 9:47-48;  Luka 6:23-25;  Luka 12:4-5;  Ufu. 14:9-11.

Pia tufikiri kidogo, kama mtu anasoma Biblia tu atakuwa na uwezo wa kukataa mafundisho ya Yesu kuhusu Jehanumu au Kuzimu?  Hapana!  Mashahidi wanatii na wanaheshima Gazeti lao juu ya Biblia ndiyo maana wanakataa.  Lakini bila ile gazeti na mawazo ya manabii wa uongo wangefuata mandiko kama yalivyoandikwa!  Ukweli ni, kwamba kuna njia mbili, moja pana moja nyembamba.  Njia nyembamba inatupeleka mbinguni na njia pana inatupeleka jehanumu!

Angalia mazungumzo katika Luka 23:43.

**Luka 22:19**

Angalia mazungumzo katika Mathayo 26:27.

**Luka 22:43**

“Yesu akamwambia, Amin, nakuambia, leo hivi utakuwa pamoja nami peponi.”  Tafsiri ya Union.

Msatari huu unaonyesha wazi kwamba watu wanaweza kuwa na ufahamu baada ya kufa.  Tunajua kutoka Luka 16 na sehemu nyingi katika maandiko, Mashahidi wanafundisha kuwa tunapokufa hatuwi na ufahamu tena, mpaka Yesu atakaporudi.  Sasa lakini Yesu alimwambia mwenye dhambi msalabani kwamba “Leo hivi utakuwa”.  Yesu alisema leo, siyo kesho, au baada ya miaka 2000.  Alisema leo.  Kwa hiyo mstari huu unaweza kutumika iliuonyesha ya kuwa Yesu aliaamini kabisa ya kuwa siku ile atamwona huyu mtu.  Sasa je!  Tuamini nani Chama Cha Mashahidi au Yesu!

Kwa miaka mingi baada ya maisha ya Charles Russell.  Mashahidi walikuwa na taabu na walifundisha kuwa baada ya kifo hatuna ufahamu kwa sababu ya mstari huu.  Lakini kwenye tafsiri yao ya maandiko walibadirisha tena maandiko ili wasaidie mafundisho yao.  Na ni jambo la shangaza ya kuwa wanadamu wanabadirisha maneno ya Mungu.  New World Translation inasema hapa, “Yesu akamwambia, Amin, nakuambia leo, hivi utakuwa pamoja nami peponi.”  Umeona tofauti?  Walifuta alama hii (,) na kuweka sehemu tofauti iliwabadirishe maana ya mstari!

Maandiko yanasema, “nakuambia, hivi leo....”
Tafsiri ya New World, “nakuambia leo, hivi.....”

Kwa hiyo wanafundisha huyu mtu hakuenda Paradiso!  Wanafundisha kuwa bado anasubili kwenda Paradiso!  Kwa sababu wanafundisha kuwa baada ya kifo hakuna ufahamu.  Na kama huyu mtu

angekwenda Paradiso siku ile na kumwona Yesu basi hadithi hii itabomoa mafundisho yao. Kwa hiyo kwa sababu mstari huu unabomoa mafundisho yao, wanabadirisha mstari tu. Wamebadirisha kidogo, lakini kidogo ni zaidi sana. Soma Gal. 1:6-9.

**Luka 24:36-39**

"Na walipokuwa katika kusema habari hiyo, yeye mwenyewe aliseimama katikati yao, akawaambia, Amani iwe kwenu. Wakashituka, wakaogopa sana, wakidhani ya kwamba wanaona roho. Akawaambia, Mbona mnafadhaika? Na kwa nini mnaona shaka mioyoni mwenu? Tazameni mikono yangu na miguu yangu, ya kuwa ni mimi mwenyewe. Nishikenishikeni, mwone; kwa kuwa roho haina mwili na mifupa kama mnavyoniona mimi kuwa nayo."

Hapa tena ni mstari ambao mashahidi wanakataa kabisa, mafundisho yao wanapinga na tena hawaamini maneno ya Yesu hapa. Katika kitabu kimoja cha Watchtower, kinachoitwa Vitu Ambavyo Mungu Haiwezekani Kusema Uongo, 1965, uku. 354, walisema, "Mwili wa mwanadamu wa kimwili, ambao Yesu Kristo alilazwa chini kwa milele kwa sadaka ya ukombozi, ulitupwa mbali na nguvu za Mungu, lakini sio kwa moto kwenye dhabihu kule Yerusalemu. Mwili wa sadaka kila mara inatupwa na inafutwa kabisa, ili isichafuliwa."

Sasa swali linakuja, tumwamini nani? Mungu au Charles Russell ambaye amesha julikana wazi ni nabii ya uongo? Tena tunajua Yesu alisema katika Yoh. 2:19, "Livunjeni hekalu hili, nami katika siku tatu nitalisimamisha." Hekalu kama tunajua ni mwili wa Yesu. Ndiyo maana Yesu alionyesha mwili wake kwa mitume wake. Hata Tomaso alikuwa na shaka, lakini baada ya kumwona Yesu alijua kabisa ya kuwa Yesu amefufuliwa na mwili wake! Mashahidi wanafundisha Yesu alifufuka lakini alifufuka roho tu. Katika kitabu cha Watchtower, Sababu Kutoka Kwa Maandiko, 1985, uku. 335, "Kufuati afufuo wake, Yesu kila mara hakuonekana katika mwili ule wa kimwili."

Mashahidi wa siku hizi wanahitaji kuchagua, kuamini Yesu au shirika la wanadamu fulani.

**Yohana 1:1**

"Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu."

Tangu mwanzo wa dhehebu la Mashahidi walikuwa wanabeba tafsiri ya Biblia (American Standard) ilivyoandikwa sawa na Union ya Kiswahili. Lakini kwa sababu Mashahidi walishindwa kufundisha mambo mengi kwa sababu tafsiri waliyokuwa wanatumia ilipinga mafundisho yao, walianza kuandika Biblia yao. Na siku hizi tunajua kupitia Mashahidi ambao walikuwepo, watu wengi ambao walisaidiana kuandika tafsiri yao hawakuwa watalam wa lugha za Kiebrania, Kiyunani na Kiarabu.

Hapa katika Yoh. 1:1, Mashahidi walibadirisha katika tafsiri yao. Hata hivyo walibadirisha lakini ukweli bado unabaki pale pale. Mashahidi wanafundisha Yesu ni miungu kati ya miungu wengi (1 Kor. 8:5; 2 Kor. 4:4). Na kwenye tafsiri yao ya New World wametafsiri Yoh. 1:1 inasema, "Naye Neno alikuwa miungu." Walibadirisha neno "Mungu" na kuweka "miungu". Bila kufuata lugha ya Kiyunani, bila kufuata ukweli walibadirisha tu! Kwa sababu ilikuwa ina pinga mafundisho yao. Na kwa sababu ya kiburi chao walishindwa kubadirisha mafundisho yao kwa hiyo wanabadirisha maneno ya Mungu!

Lakini kuna sehemu mbali mbali zinazonyesha na kuthibitisha hata kwenye tafsiri yao ya kuwa Yesu ni Mungu.  Katika Yohana 20:28 wakati Tomaso alipomwona Yesu alisema, “Bwana wangu na Mungu wangu.”  Isaya 9:6, “Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, Tumepewa mtoto mwanamume;  Na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake;  Naye ataitwa jina lake, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani.”

Na kama kuna mtu anaamini Baba ni Mungu wakati Yesu ni “miungu” anatakiwa kusoma katika kitabu cha Isaya 43:10-11 na 44:8, “...Kabla yangu hakuumbwa Mungu awaye yote, wala baada yangu mimi hatakuwapo mwingine.  Mimi, naam, mimi ni Bwana, zaidi yangu mimi hapana mwokozi.....hakika hapana Mwamba; mimi sijui mwingine.”  Huyu “Mwamba” ni nani?  Mat. 16:18, “Na juu ya Mwamba huu nitalijenga Kanisa langu.”

**Yohana 3:3, 7**

“Yesu akajibu, akamwambia, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu....Usistaajabu kwa kuwa nilikuambia, hamna budi
kuzaliwa mara ya pili.”

Mashahidi wa Yehova hawaamini kama wanatakiwa kuzaliwa tena.  Wanadai kuzaliwa tena ilikuwa kwa wale 144,000 tu.  Lakini hawa kwenye “Mkutano Kubwa” hawana budi ya kubatizwa kwa sababu watarithi ulimwengu huu.  (Angalia mazungumzo katika Ufu. 7:4, 9, kwa imani yao kuhusu 144,000).  Watchtower, 15/2/86, uku. 14, “ ‘Kondoo zingine’ hawahitaji kile kitu cha kuzaliwa tena, kwa sababu mwelekeo wao ni maisha ya milele katika paradiso ilifanywa upya katika ulimwengu huu na watakuwa chini ya Ufalme.”  Kwa hiyo Chama Cha Mashahidi kinafundisha wazi kwamba watu hawahitaji kubatizwa.  Tena wanapinga mafundisho ya Yesu!

Ili kuonyesha kuwa Mashahidi wamekosea hapa uanzee hapa, Yoh. 3:3-15.  Baada ya kusoma hapa sititiza mstari wa 3, “Mtu asipozaliwa mara ya pili.”  Yesu hakuwa ana ongea kuhusu kikundi cha watu hapa, alikuwa ana ongea kuhusu watu wote.  Baada ya hapa, nenda 1 Yoh. 5:1, “Kila mtu aaminiye kwamba Yesu ni Kristo amezaliwa na Mungu.”  Baada ya kusoma hapa mwuliza huyu mshahidi, “Kila mtu aaminiye” Ina waacha wengine nje?  Halafu, uende katika Gal. 4:5-6, “Kusudi awakomboe hao waliokuwa chini ya sheria, ili sisi tupate kupokea hali ya kuwa wana.  Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, aliaye, Aba, yaani, Baba.”  Tena uliza huyu Msahidi, “Je! Umewai kupokea hali ya kuwa wana na kupokea Roho?”  Sasa hapa Mshahidi huyu atajibu, “Hapana,” kama anaamini mafundisho yao.  Halafu mpeleke katika Rum. 8:14-16, na umwonyeshe mistari hii inayofundisha kuhusu kumpokea Yesu na Roho.  Na huyu Mashahidi kama anaamini mafundisho yao atasema, “Hapa haizumguzi mimi”.  Baada ya hapa mpeleke huyu hapa hapa kwenye mstari wa 8-9, “Wale waufuatao mwili hawawezi kumpendeza Mungu.  Lakini ikiwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu, ninyi hamfuati mwili;  bali mwaifuata roho.  Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake.”

Bada ya kusoma hapa, mkumbushe huyu mashahidi ya kuwa alikwisha kubali kwamba hakupokea Roho wa Kristo na kukaa ndani yake kupitia kuzaliwa upya.  Kwa hiyo kufuatana na mistari ya 8-9 kama hajapokea Roho basi yeye ni wa mwili na hawezi kumpendeza Mungu.  Sasa ukifika hapa, atakubali au kubisha.  Lakini maandiko ni rahisi, kama hatuna Roho wa Kristo basi hatuna Mungu.  Na hatuwezi kupokea Roho bila kuzaliwa upya.

**Yohana 4:23**

"Lakini saa inakuja, nayo sasa ipo, ambayo waabuduo halisi watamwabudu Baba katika roho na kweli. Kwa maana Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu."

Mstari huu ndiyo mtego wa Mashahidi, usikamatwe hapa! Kwanza wanapiga hodi. Pili, unawakaribisha. Tatu, wanauliza, "Je! Unamwabudu nani kama Mungu?" Ukijibu Mungu au Bwana, watasema, "Neno Mungu ni cheo." Watauliza tena, "Je! Jina la Mungu ni lipi?" Na wengi watajibu, "Yesu". Ukijibu "Yesu", Mashahidi watafungua hapa katika Yohana 4:23 na kusoma, "Watamwabudu Baba." Halafu atasema, "Wewe humwabudu kwa kweli kwa sababu unamwabudu Mwana sio Baba." Kwa hiyo naona umekwishaona mtego wao mmoja.

Mashahidi kwa kweli wanamkataa sana Yesu na kufundisha Yehova tu ndiye anastahili kuabudiwa. Kwa kuthibitisha haya watakupeleka wewe kwenye mistari mengi na kutumia bila mazingira yao. Pia hawasomi, Isa. 9:6; Mat. 28:9; Yoh. 1:1; Yoh. 8:58-59; Yoh. 20:28; Kol. 2:9; Ebr. 1:6 na kuendelea.

Sasa kama unataka kumtega Mashahidi hapa hapa kwanza kubali kwamba tunatakiwa kuabudu Yehova (kwa sababu ni kweli); pia uliza, "Je! Unaheshimu mapendekezo ya Baba?"
62

Atajibu "Ndiyo". Halafu mpeleka katika Yoh. 5:23, "Ili watu wote wamheshimu Mwana kama vile wanavyoheshimu Baba, Asiyemheshimu Mwana hamheshimu Baba aliyempeleka." Kama Mashahidi anakataa kumheshimu Mwana kupitia ibada kama anaheshimu Yehova, basi hafuati matakwa ya Baba, na haheshimu Baba pia!

**Yohana 6:53**

Angalia mazungumzo katika Mat. 26:27.

**Yohana 8:58**

Hapa tunaona Yesu alikuwa ana jibu swali la Wayahudi. Na alikuwa na maana kuwa yeye ni wa milele. Na alitumia maneno yale yale katika Kutoka 3:14, "Mungu akamwambia Musa, Mimi niko ambaye niko, akasema, ndiyo utakavyowaambia wana wa Israeli; Mimi niko amenituma kwenu." Na Wayahudi waliposikia maneno yale walitaka kumpiga mawe Yesu Kristo. Hata adui wa Yesu walielewa maneno ya Yesu hapa.

Mashahidi hawataki kuona mahali kwenye Biblia panapo onyesha Yesu anadai yeye ni Mungu. Lakini hapa Yesu anasema na anaeleza tena yeye ni sawa na Baba.

Kwa mazungumzo zaidi angalia Kutoka 3:14.

**Yohana 10:16**

"Na kondoo wengine ninao, ambao si wa zizi hili; na hao nao imenipasa kuwaleta; na sauti yangu

wataisikia;  kisha kutakuwako kundi moja na mchungaji mmoja."

Hapa Mashahidi wanadai "kondoo wengine" ni watu tofauti na wale 144,000 ambao walijawa na Roho. Na wanadai lile "kundi ndogo" (144,000) ni wale kwenye Luka 12:32.  Tena wanafundisha kwamba kutoka 1935 hakuna tumaini kwenye ile kundi dogo.

Lakini Mashahidi ambao wanafundisha leo hawa ndio hawana tumaini kule mbinguni, wanayakataa tena mafundisho ya Yesu Kristo Mwana wa Mungu na Mungu mwenyewe.  Angalia mazungumzo katika Ufu. 7:4 na 7:9 kuhusu mafundisho ya 144,000.

Pia angalia mazungumzo katika kitabu cha Zab. 37:9, 11, 29;  115:16;  Luka 23:43 na Ufu. 7:9.

"Kondoo wengine" kufuatana na mawazo ya Yesu ni Mataifa.  Tuna jua kwa miaka mingi sana na kupitia Agano la Kale, Mungu alikuwa na taifa teule.  Na wale watu walikuwa Wayahudi.  Lakini sasa Yesu amekuja kwa watu wote na lile "kundi lingine" ni mataifa.  Soma Mdo. 10-11;  18:10.  Pia ukiangalia katika kitabu Efeso 4:4, kuna mwili mmoja tu.  Sasa Mashahidi wanafundisha kuwa kuna miili.  Lakini siyo Yesu na Paulo walisema,  kuna mwili mmoja, na mwili huu umefanywa na watu wote wa dunia kwa sababu Baba alimtuma Mwana iliawaokoe watu wote.  Siyo ile kundi dogo tu la Wayahudi.

**Yohana 14:28**

"Mlisikia ya Kwamba mimi naliwaambia, Naenda zangu, tena naja kwenu.  Kama mngalinipenda, mngalifurahi kwa sababu naenda kwa Baba, kwa maana Baba ni mkuu kuliko mimi."

Mstari huu ndiyo mstari wanao upenda wa Mashahidi.  Ili wafundishe ya kuwa Yesu sio Mungu kwa sababu Baba ni mkuu kuliko yeye.  Na hapa tena wanatumia mstari bila mazingira ya Biblia.  Kwa sababu mazingira ya Biblia ni:

1) Yesu ni Mungu, Yesu na Baba ni umoja.
2) Lakini baada ya kuchukua mwili wa mwanadamu na kufika hapa alishushwa chini ya Baba pamoja na Malaika!

Filipi 2:6-7, "Ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho;  bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu."  Kwa hiyo hapa Paulo anafafanua kabisa kwa nini Yesu hapa ulimwenguni alikuwa chini ya Baba.  Kwa sababu alichukua mwili wa mtumwa!

Ebr. 2:9, "Ila twamwona yeye aliyefanywa mdogo punde kuliko malaika, yaani, Yesu kwa sababu ya maumivu ya mauti, amevikwa taji ya utukufu na heshima, ili kwa neema ya Mungu aionje mauti kwa ajili ya kila mtu."  Hata hapa tunaona Yesu alishushwa chini ya malaika.  Lakini Je!  Mashahidi wanafundisha Yesu ni chini ya malaika?  Hapana!  Wanadani Yesu ni Malaika Mkuu.

Kwa hiyo Biblia inafundisha kuwa Yesu alishushwa chini ya Baba na Malaika wakati alipokuja kama mwanadamu.  Lakini Mashahidi wanashika mstari mmoja tu bila kutafakari maandiko.  Kweli maandiko yanafundisha Yesu alishushwa chini.  Lakini kweli Biblia inafundisha Yesu alikuwa "SAWA NA MUNGU."  Kwa hiyo kama Pumzi ya Mungu inasema Yesu alikuwa sawa na Baba, halafu akaja hapa

ulimwenguni;  Je!  uko tayari kukataa maandiko wakati ni wazi wazi?

Pia angalia mazungumzo katika Isa. 9:6; Yoh. 1:1; Yoh. 20:28; na Ufu. 1:7-8.

**Yohana 16:13**

"Lakini **yeye ata**kapokuja, **huyo** Roho wa kweli, **ata**waongoza awatie kwenye kweli yote;  kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote **ata**kayoyasikia **ata**yanena, na mambo yajayo **ata**wapasha habari yake."

Mistari ya 7-15 katika sura ya 16 ni mistari mizuri sana wakati unaongea na Mashahidi kuhusu Roho Mtakatifu.  Kama tunaelewa Mashahidi wanakataza na kudai Roho sio nafsi ya Mungu bali ni nguvu fulani.  Kwa hiyo wanadai Roho sio nafsi bali ni kitu.  Lakini ukisoma hapa katika mstari wa 13 utaona Yesu anaongea kuhusu "Yeye", sio kuhusu "Kitu".  Maneno ya lugha yanasema, "Yeye, ata-";  maneno "yeye, ata" yanasimamia mtu au nafsi sio kitu.  Tena tunaona hapa Roho anaongea, anasikia, anamwambia, matendo, hali na sifa ya mtu au Mungu!

Kwa hiyo mistari hii inaonyesha Roho ni mtu na anasifa za mtu, kama unataka mistari na mazungumzo kuhusu Roho ni Mungu soma katika kitabu hiki:  Mwa. 1:1-2;  Mat. 3:11;  Mdo. 2:4;  Mdo. 5:3-4 na 1 Kor. 6:19.

**Yohana 17:3**

"Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma."

Mashahidi wanatumia mstari huu katika njia mbili.  Njia ya kwanza ni wakati wanatembea nyumba kwa nyumba watasoma mstari huu na kusema;  "Kama unataka kujua Mungu, basi chukua masomo haya na kusoma na utafahamu Mungu."  Hii ndiyo ngazi ya kwanza ya kufundisha mtu ya kuwa Gazeti na masomo yao ni muhimu kuliko maandiko.

Kwa sababu wanadai kabisa, "kama unataka kumjua Mungu, chukua makalatasi haya".  Na kweli kama utachukua makalatasi haya na kujifunza basi kuna maneno ya maandiko kwa ajili yako, "Wakijifunza siku zote, ila wasiweze kabisa kuufikia ujuzi wa kweli, " 2 Tim. 3:7.  Elimu ya Mungu iko kwenye maandiko siyo kwenye makalatasi na vitabu vya Watchtower.  Pia soma, 2 Tim. 3:15-17;  2 Pet. 1:3;  na Yuda 3.

Njia ya Pili wanatumia mstari huu kwa kukataa Uungu wa Yesu.  Wanaonyesha jinsi Yesu alivyosema, "Mungu wa Pekee na wa kweli."  Na wanajaribu kujenga hoja na kudai kuwa Yesu aliwekwa mbali yeye kutoka kwa Mungu.

Lakini hapa, Yesu hakuwekwa au hakutenganishwa yeye toka kwa Baba.  Na tufikiri kidogo labda Mashahidi wanaongea kweli hapa na Baba ni Mungu tu.  Basi tuangalia Yuda 4, "Kwa maana kuna watu waliojiingiza kwa siri, watu walioandikiwa tangu zamani hukumu hii, makafiri, wabadilio neema ya Mungu wetu kuwa ufisadi, nao humkana yeye aliye peke yake Mola, na Bwana wetu Yesu Kristo."  Sasa tufanyeje?  Nani ni Mungu?  Mbona anasema Bwana wetu Yesu Kristo ni Mungu.  Na ukisoma 2 Kor. 3:17 utaona Biblia inataja Roho Mtakatifu ni Bwana Mungu.  Kwa hiyo Biblia inaeleweka, kama Biblia inasema Baba ni Mungu, siyo kwamba inakataza Yesu na Roho.  Vile vile kama maandiko yanasema Yesu ni

Mungu, siyo kwamba yanakataza Baba na Roho. Tena kama maandiko yanasema Roho ni Mungu, siyo kwamba yanamkataa Yesu na Baba. Kwa hiyo kufuatana na Maandiko Uungo ni Roho, Yesu na Baba. Kwa hiyo haiwezekani Mashahidi kuongea ukweli wakati wanasema Mungu ni Baba tu. Kwa sababu tunaweza kuwapeleka kwenye mistari mingine inayoeleza kuwa Yesu ni Mungu na Roho ni Mungu pia!

**Yohana 20:25**

“Basi wanafunzi wengine wakamwabia, Tumemwaona Bwana. Akawambia, Mimi nisipoziona mikononi mwake kovu za **misumari**, na kutia kidole changu katika mahali pa **misumari**, na kutia mkono wangu katika ubavu wake, mimi sisadiki hata kidogo.”

Kama tumeshagusa kwenye kitabu hiki, Mashahidi hawaamini Yesu alikufa msalabani. Wanadai alikuwa kwenye nguzo. Na wanafundisha kama mtu anaamini Yesu alikufa kwenye msalabani basi unaamini upagani. Chama Cha Watchtower kinadai mikono ya Yesu iliinuliwa juu na waliweka mikono yake pamoja halafu waka piga msumari kwenye mikono yake.

Sasa tuangalie maneno ya **Shahidi wa Kweli**, aliitwa Tomaso. Tomaso alisema “..Nisipoziona mikononi mwake kovu za **misumari**....mahali pa **misumari**..” Tomaso alikuwa Shahidi wa Kweli. Na alisema “misumari” ilipigwa mikononi mwa Yesu sio “msumari”. Kwa hiyo maneno ya mashahidi wa kweli inaonyesha ya kuwa mikono ya Yesu hawakubandika pamoja. Lakini kila mkono ilikuwa na msumari wake. Kwa hiyo hapa tena tunaweza kuona Mashahidi wa Yehova wanataka kubadirisha maandiko ili maandiko yakubaliane na mafundisho yao. Hawataki kubadirisha mafundisho yao ili wakubali mafundisho ya Mungu na hapa hatari ipo! Soma Gal. 1:6-9.

**Yohana 20:28**

“Tomaso akajibu, akamwambia, Bwana wangu na Mungu wangu!”

Hapa tena Mshahidi wa kweli Tomaso, alimwona Yesu na akajibu maneno ya juu hapa. Na hapa kwenye mstari huu unaweza kuonyesha jinsi Yesu alivyo Mungu! Hata mitume walijua na walikili! Na Mashahidi hawapendi mstari huu hata kidogo kwa sababu unapinga mafundisho yao.

Ukimpeleka Mashahidi wa Yehova hapa mara nyingi wata kuwa na njia tatu ya kutokea kwenye mtego wako.

1) Watajaribu kuluka kwenye mstari huu bila kusema cho chote.

2) Mashahidi hawajakomaa watadai, Tomaso alishituka kwa hiyo alisema, “Mungu Wangu”. Lakini kama tunajua kusema “Mungu Wangu” wakati unashituka ni kutumia jina la Bwana bure na ni dhambi kabisa. Sasa Je! Tomaso alitumia jina la Bwana bure hapa au alikiri moja kwa moja ukweli kuhusu Yesu. Ukiona mstari wa 29, Yesu hakulalamika kwa sababu alitumia jina la Bwana bure. Bali, Yesu alifurahi ya kuwa Tomaso sasa anaamini. Kama Tomaso angetenda dhambi hapa, Yesu kama mwalimu wake angemfundisha au angemlaani Tomaso. Kwa hiyo wakati Tomaso alimwona Yesu, alishangaa ndiyo, lakini alikiri moja kwa moja, “Bwana wangu na Mungu wangu.” Hakusema, “Mungu wangu” tu!

Hapa Mashahidi hawataki kukataa maandiko tu, lakini pia wanataka kumhukumu Tomaso kwa jibu lake

wakati Yesu hakumhukumu.

3) Kwa Mashahidi ambao wamekomaa kidogo watakupeleka katika mstari wa 31, “Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu.” Kwa hiyo kwa sababu Baba ni Mungu na Yesu ni Mwana wa Mungu wanadai Yesu sio Uungu. Tena wanaweza kurudi katika Yoh. 20:17.

Lakini usiwaache waruke ruke kama wamekanyaga msumari.

Wabane hapo hapo kwenye maneno ya Tomaso kisha wapeleke katika Ebr. 1:10, hapa Mungu anajiita Yesu “Bwana”. Je! Mungu anamwita Yesu “Bwana” kwa sababu Yesu ni mkubwa zaidi? Hapana! Alimwita Yesu Bwana kwa sababu Yesu ni Bwana kama Baba ni Bwana, Yoh. 17:11.

Pia kwa msaada zaidi angalia Mwa. 18:1-2; Isa. 9:6; Dan. 10:13, 21; 12:1; Yoh. 1:1; na Ufu. 1:7-8.

**Matendo 1:5**

Angalia mazungumzo katika Matayo 3:11.

**Matendo 2:4**

“Wote wakajazwa na Roho Mtakatifu.”

Kwenye kitabu cha Watchtower 1982, “Unaweza Kuishi Milele Katika Paradiso Hapa Ulimwenguni,” inasema katika ukurasa ya 40-41, “Wote walijazawa na roho mtakatifu. Je! Walijazwa na mtu? Hapana, lakini walijazwa na nguvu yenye uhai wa Mungu. Kwa hiyo ukweli Uungu siyo mafundisho ya Biblia........roho mtakatifu anawezaje kuwa mtu, wakati alipowajaza wanafunzi 120 wakati mmoja?”

Kama Roho Mtakatifu siyo mtu kwa sababu alimimina basi hata Paulo siyo mtu! Katika Fil. 2:17, Paulo alisema, “Naam, hata nikimiminwa juu.” 2 Tim. 4:6, “Kwa maana, mimi sasa namiminwa..” Kwa hiyo kama Roho Mtakatifu siyo mtu kwa sababu alimimina basi hata Paulo hakuwa mtu kwa sababu alimiminwa.

Unahitaji kusoma katika Flp. 2:17 na 2 Tim. 4:6 pamoja na mshahidi na kuuliza, “Je! Paulo alikuwa mtu au hapana, kwa sababu alimimina.” Kama Mshahidi anakubali Paulo ni mtu

70

kwa sababu alimiminwa, basi kuna tofauti gani kati ya Paulo na Roho Mtakatifu? Tofauti ni, Roho Mtakatifu ni Mungu! (Mdo. 5:3-4).

Tena angalia Efe. 1:23, kwenye maandiko.

**Matendo 5:3-4**

Ukisoma hapa na Mashahidi, unahitaji kusoma talatibu na labda mara nyingi mpaka ataelewa Roho ni sawa na Mungu. Kwa sababu Anania alisema uongo kwa Roho Mtakatifu; kwa Mungu. Je! Unawezeje kusema uongo kwa nguvu fulani? Watu wanasema uongo kuhusu kwa watu Uungu sio kwa nguvu fulani!

Pia angalia mazungumzo katika Yoh. 16:13; Rum. 8:26-27; na 1 Kor. 6:19.
Pia angalia mazungumzo katika ukurasa wa 21-22.

**Matendo 7:59-60**

"Wakampiga kwa mawe Stefano, naye akiomba, akisema, Bwana Yesu, pokea roho yangu."

Ni kosa kubwa sana kama Mashahidi watajwa Yesu Kristo katika maombi kama Stefano. Na kama watakamatwa wakati wanaomba kama Stefano watafukuzwa kutoka dhehebu hili. Lakini hapa unaweza kumbana kwa kuonyesha Stefano alipokuwa anaomba na alitaja jina la Yesu na alikuwa anaongea na Yesu. Huwezi kukataa maandiko! Lakini Mashahidi watakataa kwa sababu ni kawaida yao na watapata taabu, 2 Thes. 1:8.

**Matendo 15:28-29**

Angalia mazungumzo katika kitabu hiki kwenye Mwanzo 9:4.

**Warumi 8:8-9**

Mashahidi kwa kweli wanawachanganya watu wa leo. Kwanza wanadai hatuakolewi kupitia ubatizo lakini wanadai wanaokolewa kupitia imani tu (somo uku. 25-26). Lakini tena wanafanya kazi sana ili wajulikane na Mungu. Watatembea mpaka mwisho wa dunia ili wampendeze Mungu. Sasa je! Matendo yanaokoa au hayaokoi? Ni lazima Mashahidi wachague. Kwa sababu Mashahidi bado wako kwenye mwili na bila kujali wanafanya matendo ya kiasi gani hawawezi kuwa waaminifu kwa Mungu.

Kama unajifunza na Mshahidi kuhusu sura hii anza katika mstari wa 1 kusaoma mpaka wa 17. Pia angalia kwenye kitabu hiki maneno ya Yoh. 3:3.

**Warumi 8:26-27**

Mashahidi wa Yehova hawajawahi kusoma au kujifunza mstari huu katika ibada zao. Kwa sababu viongozi wao wanaachalia mbali mstari huu. Kwa sababu mstari hii kwa ufupi inaongea kuhusu nafsi ya Roho Mtakatifu, na kwa sababu wanafundisha Roho Mtakatifu sio nafsi ni lazima wafumbe macho kwenye mistari hizi. Tunaweza kusoma mstari wa 26 unasema, "Roho naye," "Roho mwenyewe".

Sasa omba Shahidi asome hapa na uliza maswali haya: Je! "Nguvu" fulani inaweza "Kutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa? Je! "Nguvu" fulani ina hekili? Je! Kitu ambacho sio nafsi kinaweza kufikir kuombai au kutoomba?

Kwa mistari mengine ili kumsaidia Mshahidi kwamba Roho Mtakatifu ni nafsi soma: Yn. 16:13; Mdo. 5:3-4; 1 Kor. 6:19.

**1 Wakorintho 1:10**

Chama cha Watch Tower kinatumia mstari huu ili kuthibitisha kuwa wana umoja. Mashahidi wengi

wanatii Watch Tower zaidi ya maandiko kwa hiyo wanadai kuwa wao ni wakristo wa kweli kupitia mafundisho ya Watch Tower!!

Wamelazimisha wasikubali au kusoma mafundisho ya watu wengine (Watch Tower 1/5/84, uk. 31) pia wanalazimisha wasisikia upimaji wa uzuri kuhusu Chama chao (Watch Tower 15/4/84, uk. 17). Pia wamelazimisha wasiongee maneno yo yote kuhusu jinsi wazee wanavyofanya kazi (Watch Tower 15/1/84, uk. 16). Pia wamelazimisha <u>wasifikiri wenyewe</u> na waombe sana wasifikiri kwa uhuru (Watch Tower 15/1/83, uk. 22, 27).

Je! Hapa katika 1 Kor. 1:10; Paulo alisema usifikiri? Usiwe na uhuru wa kufikiria? Au, uishi kama jiwe na kama Chama Cha Yehova kule Merakani wakiongea basi ni maandiko na huwezi kukataa au kuyajaribu mafunidisho yao? **Hapana!**

Alifundisha tusiwe na faraka! Tuongee mamoja! Je! Tuongea mmoja kupitia nani? Watch Tower au Yesu Kristo? Somo mstari wa 11-17? Je! Hapa anaongea kuhusu Watch Tower au Yesu Kristo? Anaongea kuhusu Yesu na kama Yesu hajagawanyika basi fundisho lake ni moja! Na mafundisho yake ni mamoja kwa sababu alipokea mafundisho yake kutoka kwa Baba yake. Tena Yesu na Baba yake ni wamoja (Yn. 17:11) ndiyo maana Yesu aliomba sisi tuwe na umoja katika Yohana 17 na ndio maana Paulo anasema hapa katika 1 Kor. 1:10. Anataka sisi tunena mamoja. Kwa sababu mtu moja tu alisulibiwa kwa ajili yetu msalabani na huyu mtu ni Yesu! Siyo Chama cha Watch Tower!

**1 Wakorintho 6:19**

Hekalu ni nini? Hekalu ni mali ya Mungu au miungu fulani, tena ni sehemu ya kuabudie Mwenye hekalu. Mungu katika Agano la Kale alikuwa na hekalu lake kule Yerusalemu. Wafilisti walikua na hekalu la Dagoni (1 Sam. 5:2), Watu wa Efeso walikuwa na hekalu ya Atemi (Mdo. 19:35. Kila hekalu ilikuwa mali ya Mungu au miungu ya uongo. Lakini hapa Biblia inaeleza kuwa miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu. Hekalu la nani? Roho Mtakatifu.

Kwa hiyo hapa unaweza kumfundisha shahidi kwamba sisi ni hekalu la Roho Mtakatifu anayeishi ndani yetu sio :nguvu" fulani inayoisha ndani. Na katika Agano la Kale makuhani walishindwa kuingia katika hekalu chafu, basi sisi hatuwezi kuwa wachafu au kuweka uchafu kwenye miili yetu.

**1 Wakorintho 8:6**

Mashahidi wanatumia hapa ili kuthibitisha kuwa Mungu ni mmoja na yeye ni Baba. Halafu wanasimama hapa, wanakataa kuendelea na kusoma. Lakini usiache asimame hapa tu! Ni lazima asome mstari wote. Na ukiendelea utaona kuna Bwana mmoja na huyu Bwana ni Yesu Kristo. Fuatana na mafundisho yao kama Yesu sio Baba kwa sababu kuna uungu mmoja, basi Baba sio Bwana kwa sababu Bwana ni Yesu na kuna Yesu mmoja. Sasa hapa Shahidi atashindwa kwa sababu Mashahidi wanamwita Yehova, Bwana. Lakini hapa tumesoma kuna Bwana mmoja na huyu ni Yesu.

Ukweli Yesu na Baba ni wamoja (Yoh. 17:11) na mara nyingi kwenye maandiko Mungu anajiita Bwana na tena mara nyingi Bwana ni Yesu. Ukisoma Yoh. 20:28, Tomaso akasema "Bwana wangu na Mungu wangu" kuhusu Yesu!

Kwa hiyo kama Mashahidi wanataka kutumia 1 Kor. 8:6 kwa kusema Yesu sio Mungu kwa sababu inaeleza Mungu ni Mmoja.  Basi ni lazima Mashahidi wasisema tena Bwana ni Yehova!  Kwa sababu hapa tena inaeleza kuwa Bwana mmoja ni Yesu Kristo.

Tatizo lao ni kwamba wanataka kushika kipengele kimoja kwenye mstari huu lakini ni lazima washike mazingira yote ya mstari huu.  Na kama mstari huu una maana kuna Mungu mmoja na Yeye ni Baba basi kuna Bwana mmoja na Yeye ni Yesu.

**1 Wakorintho 11:7**

Mashahidi wanatumia mstari huu ili wakatae Uungu wa Kristo.  Lakini mstari huu hausemi Yesu ni Malaika aliyeumbwa na Mungu.  Unaongea kuhusu mamlaka.

Katika familia ya wanadamu kichwa cha mwanamke ni mwanaume.  Hapa ina maana wanawake ni chombo kisichofaa?  Hapana!  Ni Mungu aliweka Mume kuwa kichwa cha Mke kwa sababu "yeye" (mwanamke) alindanganywa kwanza na mwanaume aliumbwa kwa ajili ya Mungu.  Lakini mwanamke aliumbwa kwa ajili ya mwanadamu.

Ni sawa na Uungu wa Mungu, Baba ni kichwa na Yesu ni mwanawe.  Haina maana kuwa Yesu sio Mungu. Kwa sababu Mume ni kichwa cha Mke lakini tuko sawa (Gal. 3:27-28).  Kwa mfano wa Uungu Baba anaonekana mkubwa lakini wako sawa, Yn. 17:11; Yn. 1:1, 14, 17.

**Wakolosai 1:15**

Mashahidi wanatumia mstari huu kuthibitisha kuwa Yesu sio Mungu, bali Yeye ni malaika wa kwanza aliyeumbwa na

Mungu.  Lakini maneno "Mzaliwa wa kwanza" katika Biblia ina maana nyingi.

"Mzaliwa wa Kwanza" katika maandiko ina maana mbili:
1) Mtoto wa kiume wa kwanza katika familia.
2) Cheo-nani ni mkubwa zaidi.

Ukianagalia Zab. 89:27 utaona maandiko yanasema Daudi alikuwa "Mzaliwa wa kwanza" wakati tunajua alikuwa mzaliwa wa mwisho wa Yese.  Maana ya "Mzaliwa wa kwanza" hapa ni cheo.  Alikuwa mfalme Waisraeli.

Sasa katika Kol. 1:15, maneno yale yana maana gani?  Basi tunatakiwa kuaangalia mazingira ya Kolosai sura ya kwanza.  Tukianagali mstari wa 18 tunaona kwamba mstari huu unasema, "Naye ni **Kichwa** cha mwili yaani Kanisa."  "Kichwa" hapa kina maana <u>Cheo</u>, na kufuatana na mazingira ya sura hii basi "Mzaliwa wa kwanza" katika mstari wa 15 ni kuhusu Cheo Cha Yesu.  Sawa sawa na meneno yaliyo katika Zab. 89:27.

**Wakolosai 2:9**

Ni mstari mzuri sana wa kueleza kwamba Kristo ni Mungu.  Katika tafsiri yao Mashahidi wanasema Yesu

ni <u>sawa au kama Mungu</u>. Lakini hapa unasema kwa urahisi, "Katika Yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili."

**2 Timotheo 3:15-17**

Mashahidi wananukuu mistari hii sana! Lakini kwa kweli hawaamini maneno ya hapa hata kidogo! Kwa sababu ukisoma mstari wa 15 utaona kijana Timotheo alitafuta wokovu kupitia maandiko. Lakini Mashahidi wanapinga haya, wanadai kuwa haiwezikani mtu kupata wokovu kupitia maandiko. Angalia <u>Watch Tower</u> toleo la 15/9/10 uka. wa 298, "Siyo tu, "Hata hivyo, sio tu tunatafuta lakini watu hawawezi kuona mpago wa Uungu katika Biblia tu, lakini tunaona tena, kama mtu anaweka <u>Scripture Studies</u> (Kitabu cha kufundisho cha Mashahidi, kitabu hiki kimetoka Chama Cha Mashahidi) pembeni.....na anaanza kufuata Biblia tu....baada ya miaka miwili ataingia kwenye giza." Maneno yale ni maneno ya msingi wa Chama Cha Watch Tower.

Kwanza wanadai maandiko yanatosha, lakini tena **wanakataa**! Sasa, kama Timotheo alipata wokovu kupitia kujifunza maandiko kwa nini sisi hatuwezi?

**2 Petro 1:3**

"Uwezo wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa." Haya ni maneno ya Petro yanaelekeana na maneno ya Paulo. Petro alisema Mungu alitupa "vitu vyote," lakini Charles Taze Russell na chama chake anadai kuwa ukisoma Biblia tu kwa miaka miwili utaingia kwenye giza! Yesu alisema katika Yoh. 8:32, "Utaifahamu kweli na kweli italeta uhuru." Tena katika Yoh. 17:17, Yesu anaongea kuhusu Baba na alisema "Uwatakase kwa ile kweli, neno Lako ndiyo kweli!" Sasa kama tunajua maandiko ni "Pumzi ya Mungu" (2 Tim. 3:15-17). Sasa Yesu alisema tunaweza kujua ukweli na ukweli ni neno la Baba na neno la Baba ni "Pumzi ya Mungu" na "Pumzi ya Mungu" inatakasa siku hizi. Yuda 3 inasema, "...Imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu.." Kufuatana na Mungu "Pumzi yake" inatosha. Kufuatana na Yesu, Petro na Paulo "Pumzi ya Mungu" yanatosha lakini Charles Taze Russell anakataa. Sasa, tumwamini nani Baba, Yesu, Petro na Paulo au Chama Cha Watch Tower?

**Waebrania 1:6**

Mashahidi kwenye tafisri yao ya maandiko (NWT) wanabadilisha mstari huu. Kwa sababu hawataki Yesu aonekana sawa na Baba. Katika tafsiri nzuri ya maandiko hapa inafundisha malaika wanamwabudu Yesu. Lakini Mashahidi hawataki malaika wamwabudu Yesu, kwa sababu kama wanamwabudu Yesu ina maana Yesu ni bora na tena Yesu ni sawa na Baba. Tena ukiona Yohana 5:23 imeandikwa kwamba kila mtu anatakiwa kuheshimu Yesu kama Baba! Na tukishindwa kuheshimu Yesu kama Baba inamaana hatuheshimu Baba.

Kwa hiyo kwa Mashahidi ambao hawataki kumheshimu Yesu kama Baba, watalipizwa kisasi siku moja.

**Ufunuo 1:7-8**

Hapa Mashahidi wanatakiwa kuona Yesu ni Baba Mungu au ni lazima wafumbe macho yao kufuatana na tafsiri yao ya Biblia. Mara nyingi watafumba macho yao. Mistari hii inatufundisha kuwa Yesu na Baba ni wamoja, kufuatana na tafsiri yao ya New World Translation. Kwa hiyo kwa pointi hii unahitaji kuwabana

mashahidi kwa kutumia tafsiri yao. Kama huna unatakiwa kutafuta. New World Translation ya Ufunuo 1:7-8, "Tazama! Yeye atakuja na mawingu, na kila jicho litamwona, na wale waliomchoma, na makabila yote ya ulimwengu wataomboleza kwa ajili yake. Naam, Amina. Mimi ndiyo Alfa na Omega, anasema Yehova Mungu, 'aliyeko na aliyekuwako na atakayekuja, Mwenyezi.'"

Katika mstari wa 7 tunasoma, mtu atakuja. Nani atakuja? Mstari wa unasema ni mtu aliyechomwa. Nani aliyechomwa? Yesu Kristo! Tena mstari wa 8 unasema Yehova Mungu atarudi? Sasa nani atarudi? Yehova Mungu au Yesu? Mbona Yehova Mungu hajawai kuishi na sisi? Sasa atarudije? Kwa sababu unarudi katika sehemu uliowahi kufika. Sasa nani atarudi Yesu au Baba? Labda wote wawili watarudi? Hamna, mstari wa 8 unasema "Atakuja", "a" nafsi ya tatu umoja-yeye, "ta" wakati ujao. Sasa naona umeona jinsi tafsiri yao inavyopinga hapa. Tunajua mtu mmoja atarudi, sasa ni nani? Tunajua ni Bwana Yesu lakini kufuatana na mistari hii ya tafsiri ya New World Translation haieleweki!

Ufunuo 1:8 inaeleza kwa urahisi kwamba Yehova Mungu ni Alfa na Omega. Na Alfa na Omega atakuja. Sasa tuangalie Ufu. 22:12-13, "Tazama, naja upesi....Mimi ni Alfa na Omega, mwanzo na mwisho." Kwa hiyo fuatana na Ufu. 1:8 Yehova Mungu atakuja upesi. Lakini angalia jibu la kwa Yesu na Yohana katika Ufu. 22:20, "Naja, Upesi," "Amina na uje, Bwana Yesu." Nani atakuja upesi? **Bwana Yesu**!! Bwana Yesu ni Alfa na Omega, Ufu. 22:12-13, kwa sababu ni Bwana Yesu atakaerudi. Sasa Mashahidi wanajaribu kusema Alfa na Omega hapa katika sura ya 22 ni Yehova Mungu, lakini Yehova Mungu hawezi kurudi kwa sababu hajawi kuishi hapa; tena Yohana alifafanua sana Alfa na Omega hapa ni nani! Alisema, "**Amina na uje, Bwana Yesu**"!

Kwa hiyo tumeona:
1:7-Mtu atakuja.
1:7- Mtu aliyechomwa.
1:8-Yehova Mungu atarudi.
1:8-Yehova Mungu ni Alfa na Omega.
22:12-Naja Upesi.
22:12-Yule ambaye atakuja upesi ni Alfa na Omega.
22:20-Naja Upesi, Bwana Yesu!

Nani atakuja upesi (22:20)? BWANA YESU (22:20)! Yesu atakuja upesi. Na yule atakaekuja ni Alfa na Omega (22:12). Alfa na Omega atakuja upesi (22:12). Alfa na Omega tena ni Yehova Mungu (1:8). Nani anakuja upesi? BWANA YESU (22:20). Kwa hiyo ule ambaye atakuja upesi ni Bwana Yesu tena Yehova Mungu tena Alfa na Omega. Bwana Yesu ni Bwana Mungu na Bwana Yesu pamoja na Bwana Mungu ni Alfa na Omega.

Lakini tusiishie hapa, tuangalie Ufunuo 2:8. "Haya ndiyo anenayo yeye wa Kwanza na wa Mwisho, aliyekuwa amekufa, kisha akawa hai." Sasa nani amekufa na sasa ni hai? Bwana Mungu au Bwana wetu Yesu Kristo? Yesu Kristo ndiyo jibu sahihi hapa. Yesu ni wa Kwanza na wa Mwisho. Mwanzo na Mwisho ni yule atakayekuja tena. Na yule atakayekuja tena ni Yesu! Tukiangalia 1:8 imeadikwa Yehova Mungu atarudi tena Yeye ni Alfa na Omega. Je! Biblia inapingana hapa? Hapana! Yehova Mungu na Yesu ni Wamoja! Yohana 17:11.

Pia soma Ufu. 1:17-18; Isa. 48:12-13; Isa. 43:10-11 na Kol. 2:9.

Ufu. 1:17-18, “Usiogope, mimi ni wa Kwanza na wa Mwisho, na aliye hai, nami nalikuwa nimekufa, na tazama ni hai.” Biblia inathibitisha mara kwa mara kwamba Yesu na Baba ni WAMOJA!

**Ufunuo 3:14**

Mashahidi wanatumia mstari huu ili waonyeshe kwamba Yesu aliumbwa na Mungu. Kwa hiyo wanadai Yesu sio Mungu kwa sababu yeye ni mwanzo wa uumbaji. Na wanadai Yesu aliumbwa kwa sababu Ufu. 3:14 inasema yeye ni “mwanzo”. Lakini ni lazima wawe waangalifu katika lugha ya Ki-yunani, kwa sababu Mashahidi wanadai katika Ufu. 21:6 na 22:13 kwamba Baba siyo Yesu anaeongea hapa. Hapa Baba anasema Yeye ni Mwanzo. Kwa hiyo kama neno “mwanzo” ina maana aliumbwa na kitu basi hata Baba aliumbwa na kitu. Kwa sababu Baba anadai yeye ni Mwanzo, fuatana na mafundisho yao.

Lakini kwa kweli neno la Ki-yunani kwa “mwanzo” ni “arche”. Katika Vines Expository Dictionary of N.T. Words neno “arche” ina maana: “mwanzo,” “nguvu,” “mhukumu,” na “kiongozi.” Neno “arche” katika Luka 12:11 imetafisiriwa “mamlaka.” Na inamaana mtu anayetawala. Ndiyo maana tafsiri nyingi za Biblia zinasema katika 3:14, “Kiongozi cha kuumbwa kwa Mungu.” Kwa kweli Yesu alikuwa “arche” (mamlaka au nguvu) ya uumbaji ya Mungu. Yesu hakuwa kitu cha kwanza kuumbwa.

Kwa hiyo msingi hapa wa kusema Yesu aliumbwa haupo. Kama unasema Yesu aliumbwa kwa sababu ya neno “arche” basi hata Baba aliumbwa kwa sababu Mashahidi wanadai Baba ni “mwanzo” katika 21:16 na 22:13.

Kwa hiyo Yesu ni Mwanzo na Mwisho, tena ni kiongozi au nguvu au mhukumu au mamlaka ya vitu vyote vilivyoumbwa. Pia soma Kol. 1:15.

**Ufunuo 7:4**

Chama Cha Watch Tower kinafundisha kwamba kiasi cha Wakristo au kiasi cha watu wenye mwili ni 144,000 tu! Na wanadai mavuno ya wale watu yalianza katika karne ya 19 mpaka mwaka wa 1935. Na katika 1935 mavuno yaliisha na milango ya mbinguni imefungwa. Na waamini wapya tangu mwaka wa 1935 wanafanya kundi jipya linaoitwa “Mkutano Mkubwa”. Na wanafundisha kuwa wale 144,000 tu wanatumaini la kuingia mbinguni na wale tu watashiriki mkate wa milele na kikombe chake.

Kama tunavyojua kitabu cha Ufunuo kina mifano mingi. Na watu wa leo hawana umoja kuhusu mafundisho ya mifano tunayoipata hapa. Lakini, tunaweza kuthibitisha kwa Mashahidi kwamba Chama Cha Watch Tower wanakosea kusema watu 144,000 tu watarithi ufalme wa mbinguni.

Ufunuo 7:4 inasema 144,000 ni “Wana wa Israeli,” lakini Watch Tower wanasema “Wana wa Israeli” ni “Israeli ya kiroho” maana yao ni 144,000 watatokea katika mwaka wa 33 mpaka 1935 bk.. Kwa maana hiyo makabila yale hayamo kwenye hesabu hii. Lakini ukiendelea na kusoma hapa kwenye maandiko utaona 12,000 wametoka katika kila kabila la Israeli (7:5-8). Hapa makabila ya Israeli yameelezwa moja kwa moja hatuwezi kukataa haya. Watu 12,000 mara makabila kumi na mawili ya Israeli ni sawa na 144,000 (12,000 X 12 = 144,000). Kwa hiyo Biblia inaeleza wazi wale 144,000 watatoka wapi. Sasa kama number yake ni ya mifano Mungu anajua, lakini kama number moja ni ya mifano basi namba zote ni za mifano.

Mashahidi wa leo watadai numberi 12,000 ni mfano lakini 144,000 ni ya kweli. Lakini haiwezekani kwa sababu imeandikwa hapa 12,000 x 12 = 144,000. Kama number 12,000 ni mfano basi namba zote ni mfano.

Ni lazima Mashahidi waongee ukweli kuhusu yote. Siyo kuchagua namba moja kama ni ya kweli lakini number zingine katika mazingira haya wanadai ni mifano. Kama number 12,000 ni mfano basi 144,000 ni mfano. Hakuna cha kuchagua.

**Ufunuo 7:9; 19:1**

Chama cha Watch Tower kinafundisha katika mwaka wa 1935 Mungu aliacha kutia watu kwenye tumaini la mbinguni pamoja na Kristo. Wanasema katika mwaka ule Yesu alianzasha kikundi cha pili cha waumini. Na tumaini lao ni kuishi hapa ulimwenguni katika mwili wa Yesu. Kikundi cha pili cha watu kinaitwa "Mkutano Mkubwa" au "Makutano Mengi" fuatana na mistari hii ya juu.

Haya ndiyo mafundisho yao makuu yanoyafundishwa na Chama cha Watch Tower. May 31, 1935 J.F. Rutherford (Raisi wao siku zile) alidai kuwa aliona "Nuru; ikipanda juu" na siku ile anadai alipata "Ufafanuzi wa ukweli wa Uungu." Na "Nuru" ilisimamia "Mkutano Mkubwa". Hapa ndiyo chanzo cha mafundisho yao ya kuamini kuwa watarithi ulimwenguni. (Watch Tower 1/3/85 uk. 14 na 1/2/82 uk. 28).

Kwanza, hakuna fundisho la Biblia linaloeleza kwamba Yesu atakuwa na kundi la pili la watu hapa ulimwenguni. Agano la Kale ilikuwa kwa Waisraeli na Agano Jipya kwa Wakristo tu, mpaka Yesu atakaporudi tena.

Pili, Yesu hajawahi kusema katika Agano Jipya kundi la pili litakuwepo. Na kama mafundisho ya Rutherford ni kweli kwamba kuna kundi la pili, basi wale walio katika kundi la pili:

Hawawezi kuwa washiriki wa mwili wa Yesu-1 Kor. 12:20.
Hawawezi kuzaliwa tena-Yn. 3:3.
Hawawezi kujiunga na ufalme wa Mbinguni-2 Tim. 4:18.
Hawana ruhusa ya kushiriki meza ya Bwana-1 Kor. 10:16-17.
Hawamo kwenye Agano Jipya lililofanywa na Kristo-Ebr. 12:24.

Ndio maana hawafuati maandiko. Kwa sababu wanawaamini Russell na Rutherford zaidi ya Yesu na Mungu. Mungu anasema siku hizi anaongea nasi kupitia mwanawe, Ebr. 1:1-3, sio kupitia Chama cha Watch Tower.

Hata hivyo, somo 7:9 na 19:1; "Mkutano Mkubwa" au "Makutano Mengi" watasimama wapi? Mbele ya kiti cha enzi! Na mkutano huu wataongea sauti kuu; wataongea sauti kuu wapi? Mbinguni! Mistari hii miwili inaongea kuhusu watu wa Mungu waliokoolewa kule mbinguni, siyo hapa ulimwenguni.

Ndugu zangu, "Mkutano Mkubwa" ambao Mashahidi wanaamini ni wao na watarithi hapa ulimwenguni haupo kwenye maandiko! Mkutano wa watu katika mistari ya 7:9 na 19:1 ni watu kule mbinguni kufuatana na maandiko!

# Sura Ya Sita

## Hitimisho

Ni tumaini langu kitabu hiki kitasiadia kubomoa mafundisho ya mashahdi. Kwa sababu wale watu wana matatizo sana. Hawaamini Yesu ni Mwana wa Mungu lakini wanaamini mafunidisho ya watu. Wanaweka mbali Biblia na kufuata na kutafuta Chama cha Watch Tower kule Merakani. Chama kile ni wanadamu ambao wanakaa na kutengenza sheria zao tu. Na wale watu wanaweka sheria halafu kesho wanafuta. Sasa kwetu sisi wa siku hizi tukiweka imani yetu katika wanadamu tutaanguka, 1 Kor. 2:5; Yer. 17:5-7; Gal. 1:6-9.

Pia Yohana alituambia tuwajaribu walimu wote ili tuone kama wametokana na Mungu katika 1 Yoh. 4:1. Na kweli tumeshaona mafundisho mengi yao yanapinga Maandiko. Kwa hiyo kama malaika au mtu mwingine analeta mafundisho mageni, acha tu, kwa sababu atalaaniwa, Gal. 1:6-9.

85